

MSIKIENI YEYE



Asante sana, ndugu.

² Mwaweza kuketi. Nina furaha sana kuwa hapa kanisani tena usiku wa leo, ambapo sisi . . . Kanisa hasa si jengo la kanisa, bali kanisa ni mahali watu wamekusanyika. Nasi tunamtumainia Bwana Mungu ya kwamba atatupa baraka Zake kuu za namna nyingi usiku wa leo.

³ Na kwa hiyo, nilikuwa nikiwazia kwenye . . . jana juu ya kuwa na siku kumi za ibada, nami naona wanaanza kuwarudisha wagonjwa tena. Sasa, ni vipi, wangapi wangetaka kuwa na ibada ya uponyaji kesho usiku? Je, mngevutiwa na uponyaji mwingine? Hilo ni sawa. Vema, basi tutawaagiza wavulana wagawe kadi za maombi mapema kesho alasiri, ama kesho jioni, hasa, yapata . . . (Mnaanza saa ngapi? Saa moja ndipo mnapofungua.) Yapata saa moja kesho alasiri.

⁴ Halafu tuone ni watu wangapi wanaoweza kutoka, sasa, kwa ajili ya ibada ya kuwaombea wagonjwa, nasi tutafanya kila tuwezalo kumwombea kila mtu tunayejua kumwombea, ama, tunayeweza kumwombea.

⁵ Na sasa, jana jioni tulikuwa tukizungumza juu ya nidhamu kanisani. Nami nafikiri, kama tungeweza tu kuliweka kanisa katika mtazamo halisi wa kiroho, basi kutakuwa na u—uamsho, kweli, na itakuwa bora zaidi kwa maombi yetu kwa ajili ya wagonjwa. Maadamu hali ze—zetu zinaporomoka, basi ha—hatuonekani tu kuichukua jinsi inavyotupasa, lakini wakati kila mtu ameomba tu kabisa, na kuchochewa sana, na matarajio makubwa, nimeenda jukwaani na mara nyingi kuna watu elfu tano na sita, saba, na kusiwe mtu mmoja mnyonge aliyesalia mara tu ulipoingia jukwaani. Kila mmoja anainuka kutoka kwenye viti vya magurudumu, na vitanda vya wagonjwa, na machela, na kadhalika, wanaondoka moja kwa moja, kwa sababu wao tu, wako chini ya matarajio makuu sana.

⁶ Sasa, hiyo ilikuwa ni katika siku za mwanzoni mwa huduma, kabla hapajakuwapo na mtu yeyote mwingine hudumani. Nayot, kwa namna fulani imeshushwa kwa muda kidogo. Na kwa hiyo basi, kila mtu alikuwa, ilikuwa ni mpya, nao watu walikuwa tu wakitarajia chochote. Sasa, kama mngekuwa na matarajio yale yale, mtapata matokeo yale yale, yale yale, kwa sababu Mungu Ndiye awaponyaye wagonjwa. Mnaona?

⁷ M—mtu asingeweza kuwaponya wagonjwa, kwa sababu haiko katika nguvu za mwanadamu kuwaponya wagonjwa, daktari hana mamlaka ya kuponya wagonjwa. Daktari hawaponyi wagonjwa, yeye hutoa tu usaidizi kwa wagonjwa, Mungu huponya wagonjwa yote, mnaona. Mnaona? Daktari

anaweza kurudisha mkono wako kama umevunjika, ama kushona mahali kama umeukata, au kuondoa jino kama ni bovu, ama kidole tumbo, lakini hawezi kuponya mahali kilipotoka. Uponyaji ni—ni—ni kuzidishwa kwa seli ambazo hukua na—na kurekebisha, na uhai wake hufanya hivyo, naye Mungu ni uhai. Na kwa hiyo, hivyo ndivyo uponyaji unavyofanywa, ni kwa neema na rehema za Mungu.

⁸ Nao mwili wa mwanadamu uko imara sana, kama ungeninii... Mungu alijua ya kwamba tutapata ajali, na alijua ya kwamba tungekatwa, na kadhalika. Niliambiwa muda fulani uliopita na tabibu, naamini ndiye, kwamba upasuaji huu mpya wa moyo walio nao, ambapo wanaweka hizo vali za plastiki kwenye moyo wakati zimeliwa kama vile na homa ya baridi yabisi, ambapo siamini kuna mahali pengine mwilini mwako ambapo wangeweza kufanya hivyo, mahali pale tu ambapo vali hiyo ya plastiki ingefunikwa na ateri zingine moyoni, ambapo ingeshika namna hiyo na kushikilia, sehemu zingine mwilini zingeisukuma nje mara moja. Mnaona, Mungu alijua ya kwamba upasuaji huo ungehitajika.

⁹ Kama ungeukata mkono wako, ukate ateri hizo vipande viwili... Na kama, kwenye bomba la maji, uki—ukifunga bomba la maji mahali fulani mjini, angalia, kitu fulani hakina budi kulipuka, mahali fulani, yatarudi nyuma. Lakini Mungu ameipanga hivi kwamba damu hiyo itakwepa hapo, na iendelee vivyo hivyo; kama siuyo, ingerudi moyoni mwako, nayo ingekuua katika sekunde moja tu, kama ukiwahi kukata mshipa ulio mdogo sana, ungekuua katika sekunde moja tu. Lakini Mungu alijua ya kwamba tungeumia, na kadhalika, kwa hiyo Yeye—Yeye akaiaandaa miili yetu kwa kusudi hilo. Kwa hiyo sasa, tu—tunataka kujua ya kwamba yote ni wema wa Mungu.

¹⁰ Na kama vile Ndugu yetu mwema Oral Roberts ameliweka vizuri, “Mungu ni Mungu mwema.” Hakika ndivyo alivyo. Na sasa, tunajua Yeye ni Mungu mwema, bali hatutaki kutegemea hilo sana, kumbukeni, Yeye ni Mungu wa haki, pia, kwa sababu utakatifu Wake humfanya haki. Na sheria Zake hazina budi kutimizwa, matakwa Yake. Na kwa hiyo basi, kama Yeye ni Mungu mwema, hana budi kuwa mwema.

¹¹ Mara nyingi tunachanganyikiwa kuhusu wema ni nini, tunachanganyikiwa juu ya huruma ni nini, matendo ya huruma. Angalieni hili kwa dakika moja tu juu ya matendo ya huruma. Ni wangapi wanaoamini ya kwamba Yesu Kristo alikuwa mwenye matendo ya huruma? Mbona, bila shaka alikuwa.

¹² Sasa, Yeye alishuka akaenda kwenye birika la Bethesda, na hapo umati ulikuwa umelala. Inahitajika elfu mbili kufanya umati mmoja. Kwa hiyo, kulikuwako na umati wa watu wamelala pale, viwete, vipofu, vilema, waliopooza, walingojea kutibuliwa kwa maji. Ndipo Yesu akaangalia kote katika umati

huo wa watu, mpaka akamwona mtu ambaye, vema, hakuwa kiwete, akasema, “Ninaposhuka kwenda kwenye hili birika, mtu mwingine hushuka mbele yangu.”

¹³ Yeye, ugonjwa wake, alikuwa nao kwa muda wa miaka thelathini na minane, haungemwua, ulikuwa umedumaa, labda TB, au ugonjwa wa tezi dume, ama kitu fulani. Naye alikuwa amelala kwenye godoro, ndipo Yesu akamponya, kisha akaondoka, akauacha umati huo mkubwa wa watu waliopooza, na viwete, na walemavu, na vipofu. Hiyo ni kweli? Na hata hivyo alikuwa mwenye matendo ya huruma, Mwokozi mwenye huruma.

¹⁴ Hivi mliona yale aliyosema walipomwuliza juu ya jambo hilo katika kifungu cha 19? Yeye alisema, “Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, ila lile amwonalo Baba analitenda, ndilo atendalo Mwana vile vile.”

¹⁵ *Kuwa mwenye huruma* ni “kufanya mapenzi ya Mungu.” Na hivyo ndivyo huruma halisi ya Kikristo ilivyo, ni kufanya mapenzi ya Mungu. Tunayachanganya yote leo, tunajaribu kuweka sehemu ya kibinadamu ndani yake.

¹⁶ Kama vile katika upendo, tunajaribu kutumia upendo, upendo wa Mungu, kama tunavyoutumia upendo wa wanadamu. Huwezi kumpenda Mungu jinsi unavyompenda mke wako, huwezi kumpenda Mungu jinsi unavyompenda mumeo, au mpenzi wako wa kike, au mpenzi wa kiume, ni namna mbili tofauti za upendo. Moja... Hata katika Kiyunani, maneno ni tofauti, mojawapo unaitwa *fileo*, huo ndio upendo ulio nao kwa mkeo, upendo wa namna hiyo ungekufanya umwue mwanamume juu yake, wivu, bali upendo wa *Agapao*, ambao ni upendo wa kiungu, badala ya kumwua huyo mtu, ungekufanya uiombe nafsi yake yenye dhambi. Hiyo ni kweli. Hivyo ndivyo ilivyo tofauti.

¹⁷ Tunachanganya mambo ya kibinadamu na ya Kikristo, kipengele cha kitauwa, na ndipo tunapata tu mchafuko kutoka kwake, kwa sababu tunajua tu kwa inchi, futi, maili, na kadhalika, kwa wakia, na pauni, na kadhalika, hayo ndiyo yote tujuayo. Sisi ni watu wa wakati, Mungu ni wa Milele, Yeye hana inchi, hana maili, hana jana, wala kesho, Kwake yote ni Umilele. Nasi tunajaribu kuishusha akili kuu ya Mungu, isiyo na kikomo kwenye akili zetu finyu, zenye kikomo, na, loo, tunachanganyikiwa tu, kwa hiyo jambo bora zaidi katika kufanya, ni kusoma Neno Lake.

¹⁸ Pia kumbukeni ya kwamba Neno Lake halitajipinga Lenyewe. Nimekuwa katika huduma kwa miaka thelathini na mmoja, nami nimetoa aina yoyote ya mshahara wa mwaka mmoja kwa mtu yeyote anayeweza kunionyesha Andiko linalopinga lingine ambalo haliwezi kunyoshwa kwa Neno la

Mungu. Hiyo ni kweli. Watu wanapokwambia Neno linajipinga Lenyewe, waambie hawajui wanalozungumzia.

¹⁹ Mungu ameliandika katika mafumbo na mifano, ili aweze kulificha kwa wenye hekima na akili, na kuwafunulia watoto wachanga wanaoweza kujifunza. Yesu alimshukuru Baba kwa kufanya hivyo. Hiyo ni kweli? Kwa sababu hulijui kama kusoma gazeti, ni ufunuo wa kiroho. Nalo limefunuliwa wale wanaotaka kujifunza Hilo.

²⁰ Sasa, kamwe hutajifunza Hilo shuleni, kamwe hutajifunza Hilo kwa theolojia, halina budi kujulikana kwa ufunuo, kwa sababu Biblia nzima, na—na mpango mzima wa wokovu, ni kila kitu katika Biblia, na wokovu umewekewa msingi juu ya ufunuo wa Yesu Kristo. Mlijua hilo?

Waliposhuka kutoka mlimani, Yeye alisema, “Watu huninena Mimi Mwana wa Adamu kuwa ni nani?”

“Wengine walisema Wewe ni Eliya, Musa, na manabii, na kadhalika.”

Akasema, “Lakini nanyi mwaninena Mimi kuwa ni nani?”

Ndipo Petro akasema, “Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai.”

²¹ Akasema, “Heri wewe, mwana, Simoni, mwana wa Yona, kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba Yangu, aliye Mbinguni, amekufunulia hili. Na juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu; na malango ya kuzimu hayawezi kulishinda.”

²² Sasa, kanisa Katoliki la Kirumi linasema ya kwamba Yeye alikuwa akinena juu ya Petro, maana yake, “jiwe dogo.” Kama ndivyo ilivyo, alirudi nyuma mara tu baada ya jambo hilo, kwa hiyo mnaona mngekuwa katika kanisa la namna gani.

²³ Kwa hiyo basi, kanisa la Kiprotestanti lilisema Yeye alilijenga juu Yake Mwenyewe. Sasa, kama mtaangalia Neno, haikuwa juu Yake, Mwamba, la, ilikuwa ni juu ya ufunuo wa kiroho Wake Mwenyewe aliopewa Petro.

²⁴ Jambo lile lile lililotukia huko Edeni. Ni vipi Adamu...? Habili a—alijuaje kwamba ilikuwa ni mwana-kondoo badala ya tunda la kondeni? Ufunuo wa kiroho. Mnaona? Daima imekuwa ni ufunuo wa kiroho. “Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu; na malango ya kuzimu hayawezi kulishinda.”

²⁵ Loo, hebu niseme jambo hili usiku wa leo, Mkristo: Hapo ndipo watu wengi sana wanashindwa kuuona Ujumbe wa Mungu, hapo ndipo watu wengi sana wanashindwa kuziona zile kweli. Wao...Biblia inakuwa kitendawili kwao.

²⁶ Mtu fulani aliniambia si muda mrefu uliopita, mtu mashuhuri, loo, alisema, “Hapana shaka Yohana alikula ninii,”

ninaamini, “pilipili nyekundu, kitu fulani, ndipo akashikwa na jinamizi kwenye kisiwa cha Patimo.”

²⁷ Nikasema, “Jionee aibu! Huko ni kukufuru kusema jambo kama hilo dhidi ya Neno la Mungu.” Nikasema, “Kila sehemu yake ni mpango wa kweli wa Mungu usioghoishiwa.”

²⁸ Lakini ni—ni kujiweka tu mwenyewe kwa Roho wa Mungu, na kumwacha Yeye akufunulie Hilo, Yeye atamfunulia mtoto atakayejifunza. Tunapofikia mahali ambapo tunakiri kwamba hatujui chochote, na kumwacha tu Roho Wake atende mapenzi Yake kupitia kwetu, ndipo Yeye atatufundisha. Lakini tunapojua mengi sana hata Yeye hawezi kutufundisha, basi hatuwezi kufika popote.

²⁹ Nami ninasema leo, kama kuliwahi kuwa na wakati ambapo taifa hili linapaswa kuitwa likaombe, kote nchini, si kwa saa moja tu, la, si kwa dakika chache za maombi ya kimya mahali fulani, inahitaji mkutano wa maombi wa siku baada ya siku, juma baada ya juma, kote nchini, mpaka Mungu atakapojibu. Nasi tufunge kila chumba cha pombe, tuondoe kila kampuni ya tumbaku, tuondokane na dhambi yote iliyopo, tuwafanye wanawake wavae nguo tena, na kuwafanya wanaume watende kama waungwana, na kurudisha kanisani ile mikutano ya maombi ya mtindo wa kale kama tuliyozoea kuwa nayo, hiyo ndiyo njia pekee tutakayopata kuwa na amani.

³⁰ Nami najua hawatalifanya, mnaona, kwa sababu Biblia inasema hawatalifanya, na hawatalifanya, itatubidi tu kuukabili wakati wa mwisho. Na kwenu, enyi Kanisa usiku wa leo, jiwekeni tayari, kwa kuwa hamjui dakika wala saa ambapo anaweza kutokea.

³¹ Na tuinamishe vichwa vyetu sasa, kabla tu hatujafungua Neno la neema la Bwana wetu kusoma.

³² Kwa kweli, Baba yetu wa Mbinguni, Wewe unajua kila neno, na kila wazo limeandikwa. Nasi tunaona, leo, na mioyo yetu ina bidii kwa ajili ya Kanisa kuu la Mungu aliye hai, tunapooni ile saa ya Kuja kwa Bwana ikikaribia, na kujua ya kwamba Wewe umebashiri ya kwamba kanisa lingekuwa vuguvugu, ungelitapika kutoka kinywani Mwako, kwa sababu halikuwa moto wala baridi. Ee Mungu, hiyo ndiyo sababu m—mtumishi wa kweli wa Mungu, moyo wake unalilia uamsho.

³³ Tunawazia juu ya watu mashuhuri wanaovuka taifa siku hizi, wakiweka maisha yao yote ndani yake, yote waliyo nayo, loo, wakijaribu kuliita kanisa lirudi. Nao wananinii... Hilo ni onyo la Mungu. Pia Baba, ninaomba usiku wa leo ya kwamba, katika Jina la Bwana Yesu, ya kwamba utatuma uamsho hapa Klamath Falls, na kote nchini humu, huo utakuwa ni uamsho wa kuokoa nafsi, huo utakuwa ni uamsho wa kulichochea kanisa, hata watakatifu wote wa Mungu aliye hai wataanza kuomba na kufunga, kwa kuwa imeandikwa, “Kama watu walioitwa kwa

Jina Langu watakusanyika pamoja na kuomba, basi nitasikia kutoka Mbinguni.”

³⁴ Tujalie, Bwana, usiku wa leo kwamba hiyo hisia ya unyonge, baridi, ya kutojali ambayo watu wanaipata kanisani, kujua tu ya kwamba wanakuja kanisani, na kwamba wao ni wafuasi huko, Mungu, vunja hiyo hisia ya kale, ya kibinafsi, Bwana, na kuridhika kwa uongo. Tunaomba ya kwamba utawapa sehemu iridhishayo ya ubatizo wa Roho Mtakatifu, na kuijaza mioyo na nafsi zao kwa Moto.

³⁵ Jalia kuwe na kampeni kubwa za uponyaji na miamsho kote nchini, wagonjwa na waponywe. Tunaangalia hapa usiku wa leo juu ya watu waliolala hapa kwenye machela na vitanda vya wagonjwa, na hao walio nyuma huko kwenye kusanyiko wakiwa na ugonjwa wa moyo, kansa, Bwana, wakijaribu kukusanya imani mahali fulani wapate kuponywa, jalia wajue ya kwamba Wewe ndiwe Mponyaji wa mateso yetu yote. “Njoni Kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nitawapa pumziko.” Tujalie, Bwana, usiku wa leo.

³⁶ Na jalia hawa watu usiku wa leo, wahisi upako wa Roho Mtakatifu, jalia ushike kila moyo. Jalia uwe dhahiri sana kwetu usiku wa leo, hata hakutakuwako na mwenye dhambi mmoja miongoni mwetu, wala mtu aliyerudi nyuma. Jalia kusiwe na mgonjwa atakayesalia, ama mtu mnyonge, mwishoni mwa ibada hii. Tujalie, Baba. Libariki Neno Lako.

³⁷ Ndipo tunapozungumzia nidhamu ya kanisa, Bwana, tunaomba ya kwamba utayatia mafuta haya maneno, na ionekane kuwa nzuri machoni Pako. Kwa kuwa tunaomba, katika Jina la Yesu, na kwa ajili Yake. Amina.

³⁸ Kwa ajili ya somo usiku wa leo, ninataka kuchukua tu sehemu ya mlango wa 17 wa Mathayo, na maneno machache ya mwisho ya kifungu cha 5:

. . . *Huyu ni Mwanangu, mpendwa, . . . msikieni yeye.*

³⁹ Na kama Bwana akipenda, ninataka kutumia, ama kutoa muktadha, kutoka kwa hayo maneno matatu ya mwisho ya aya ya 5: *Msikieni Yeye*, maneno matatu.

⁴⁰ Ugeniniii . . . Kama nilivyosema jana jioni, haya ni mafungu madogo sana, lakini ndiyo yote tunayohitaji kujua, ndiyo thamani. Kama tutafanya tu jinsi fungu hili dogo linavyotuagiza kufanya, hakutakuwako na mtu mmoja aliyevunjika moyo katika jengo hili usiku wa leo, “*Msikieni Yeye*,” tu. Lolote asemalo mfanye, lifanyeni.

⁴¹ Halafu basi, kama wewe ni mgonjwa: “*Msikie Yeye*.” Kama wewe ni mwenye dhambi: “*Msikie Yeye*.” Kama unahitaji kitu: “*Msikie Yeye*.” Yeye anayo yote unayohitaji katika safari hii, anayo kwa ajili yako anangojea kukupa. Gharama tayari

imelipwa, hakuna gharama ya kulipia, “Msikieni Yeye,” tu. Msikilize Yeye, yale asemayo.

⁴² Nikiwazia juu ya maskini Maandiko hayo papo hapo ya kutosha tu, maneno hayo matatu yangetosha kutuma uamsho kote ulimwenguni, na kumwokoia kila mtu aliyeko ulimwenguni.

⁴³ Miaka kadhaa iliyopita, nilisoma makala ndogo katika gazeti lililokuwa likitangaza, ninaamini ilikuwa, petroli ya Sinclair, ama petroli fulani maarufu, nao walisema ya kwamba galani moja ya petroli ya Sinclair katika mtambo wa aina fulani, kama ingeweza kuundwa imara vya kutosha, ingeinua sfiniksi inchi kumi kutoka ardhini. Ndipo nikawazia, “Loo, jinsi kampuni ya Sinclair inavyopenda kujivunia nguvu za petroli yao! Na vile kidogo inaweza kufanya mengi sana.”

⁴⁴ Lakini niliwazia, usiku wa leo, ya kwamba tone moja la Damu ya Yesu Kristo linaweza kumwinua kila mwenye dhambi aliyeko kutoka kwenye matope ya udongo, na kuweka kila hospitali huru na magonjwa, kufunga kila jela na gereza, kuwakomboa wendawazimu na wanaoteseka kwenye kila hospitali ya magonjwa ya akili, kufanya shangwe kote ulimwenguni kwa tone moja la Damu ya Bwana Yesu Kristo.

⁴⁵ Na halafu kuja mkutanoni, na kuchagua fu—fungu dogo kama hili, kumbukeni, ninafanya hivyo kwa yote yaliyo moyoni mwangu kwa maombi, nikijaribu kutafuta yale tu ningewazia Roho Mtakatifu angeongoza kufundisha, ama kuzungumzia.

⁴⁶ Mara nyingi nimesema kama ningeweza tu kushikilia tone moja la Damu halisi ya Bwana wetu Yesu katika sinia, jinsi ningeishikilia mikononi mwangu, na kuisukuma moyoni mwangu, na kupaza sauti, “Ee Baba, sasa ninashikilia Damu ya Bwana Yesu moyoni mwangu!” Ingekuwa ni msisimko wa jinsi gani, na furaha, na baraka kwangu kushikilia, katika bilauri ndogo ama chochote kile, tone moja la Damu ya Bwana Yesu!

⁴⁷ Lakini mnajua, machoni Pake, nina iliyo kuu kuliko hiyo usiku wa leo, nimewashikilia moyoni mwangu usiku wa leo, ninyi watu, ambao ni walionunuliwa kwa Damu Yake. Aliwaza zaidi juu yenu kuliko alivyoiwazia Damu Yake Mwenyewe, kwa sababu Yeye aliitoa apate kuwatakasana na kuwaleta katika Uwepo Wake. Loo, ni mambo madogo. Si yale mambo makubwa tunayofanya, ni mambo madogo tunayoacha bila kuyafanya.

⁴⁸ Nilikuwa nikizungumza jana jioni kuhusu ile stempu ndogo ya posta. Nami nilikuwa nikisimulia kuhusu Mfalme George, hayati Mfalme George wa Uingereza, alipopitia British Columbia na akiwa huko Vancouver.

⁴⁹ Shule zote zilijitokeza kumwona mfalme. Nao Wakanada wakitaka kuwa wa kifalme kwa nanii wao, waaminifu, hasa, kwa mfalme wao, waliwapa watoto wote wadogo bendera ndogo ya Uingereza, wakasimame mtaani. Ndipo wakati mtukufu, mfalme, alipopita, wangepeperusha bendera hizi

ndogo kuonyesha ya kwamba walikuwa nyuma yake, na walikuwa raia wake. Basi walimu wakawapeleka hao jamaa wadogo wote huko nje. Ndipo baada ya mfalme kupita, watoto wote wadogo katika shule fulani wakarudi, ila maskini msichana mmoja mdogo sana.

Basi mwalimu akafadhaika sana, kwa hiyo akawaita watoto wote wakubwa zaidi, naye akasema, “Nini kilichompata maskini Martha?”

Nao wasingeweza kumwona, wakasema, “Vema, alikuwa katika kundi letu,” bali wasingeweza kumwona.

⁵⁰ Ndipo mwalimu akakimbia kwa hofu barabarani, akaanza kumtafuta huyu msichana mdogo ambaye hakurudi. Basi baada ya kila mtu kuondoka, barabara zilikuwa tupu, wakimfuata mfalme, wakiimba “Mungu umwokoe mfalme,” ndipo wakamwona maskini msichana huyu mdogo amesimama nyuma ya nguzo ya simu huku ameegemeza maskini kichwa chake mikononi mwake, akilia tu kwa maskini moyo wake wote.

Ndipo mwalimu akamnyanyua, naye akasema, “Martha, kipenzi, kwa nini unalia?” Kasema, “Hivi hukupata kumpeperushia mfalme bendera yako?”

Akasema, “Naam, Mwalimu, ni—niliweza kupeperusha bendera yangu.”

Akasema, “Vema basi, hivi hukumwona mfalme?”

Akasema, “Naam, Mwalimu, niliweza kumwona mfalme.”

Akasema, “Basi kwa nini unalia hivyo, kipenzi?”

Naye akasema, “Unajua, Mwalimu, nilimwona mfalme, ila nilikuwa mdogo sana, yeye hakuniona.”

⁵¹ Sivyo ilivyo kwa Mfalme wetu Yesu, sijali wewe ni mdogo jinsi gani, jinsi unavyofanya kidogo, huwezi kufanya jambo lililo dogo sana pasipo Yeye kujua yote kulihusu. Anajua kila huzuni ndogo, kila maumivu madogo unayopitia, kila masikitiko madogo uliyo nayo, haidhuru ni madogo jinsi gani, Yeye angali anajua yote kuyahusu.

⁵² Mnajua, Bwana wetu, Yeye hujikutanisha katika milki za wanadamu, wakati mwingine Yeye hujikutanisha katika makundi makubwa ya wanadamu, wakati mwingine Yeye hujikutanisha na wachache. Tuna kumbukumbu Yake kukutana na mia tano wakati mmoja baada ya kufufuka Kwake, halafu tuna mahali alipokutana na wale sabini, na pamoja na wale kumi na wawili, na hata na wale watatu, halafu tuna nyakati ambapo Yeye atakutana na mmoja tu. Hilo ndilo linalomfanya kuwa Mungu kwangu, ni kwa sababu Yeye ni unyenyekevu.

⁵³ Nimekuwa na majaliwa ya kusafiri sana, na kukutana na watu mashuhuri. Ninapokutana na watu wanaojaribu kuwa mashuhuri, hiyo ni kusema, sikuzote unaweza kumhesabu mtu

huyo, yeye ni bure. Watu mashuhuri, ambao, wao hujaribu kukufanya ufikiri wewe ndiwe mashuhuri, bali ni watu wanaotaka kuwa mashuhuri, kama tu utalifuatilia mpaka chini kabisa, utaona ni majivuno. Sasa, hilo si ninii . . . Sikusudii hilo kuwa fidhuli.

⁵⁴ Kundi moja la ndugu wa Kimethodisti ambao ndio kwanza wampokee Roho Mtakatifu walikuja kanisani mwangu, na, ambapo nilikuwa mchungaji, nao walikuwa ni watu mashuhuri, wakiishi huko Indiana, nao walikuwa wamesema, “Ndugu Branham, baada ya sisi kumpokea Roho Mtakatifu, tumekuwa tukisoma vitabu fulani,” kasema, “yatupasa kumngojea Bwana, na kumtafuta Bwana atuambie huduma yetu?”

Nikasema, “Msifanye hivyo hata kidogo.”

Akasema, “Vema, kile kitabu kilisema . . .”

Nikasema, “Lakini ngoja kidogo, ndugu.”

⁵⁵ Kama ukiwahi kuwachukua watu ambao wana bidii sana hata wanataka daima kuwa wakifanya jambo fulani, Mungu asingeweza kumtumainia mtu huyo. Kama utaangalia katika Biblia, mtu ambaye Mungu alimtumia, alikuwa ni yule mtu aliyekuwa akijaribu kuyatoroka yote, huyo ndiye ambaye Mungu alimtumia. Chukueni, kwa mfano, Paulo, Musa, na kadhalika, wakijaribu kuitoroka huduma yenyewe.

⁵⁶ Kama mtu ni . . . Mungu angempa mwanadamu kufanya jambo fulani, naye alikuwa na bidii sana nalo, muda si muda mwajua angejivuna *sana*. Lakini kama mtu hataki kufanya hilo, labda Mungu anaweza kumtumia kwa kitambo kidogo, kwa vyovyote vile, kama tu unaweza kupata kitu kutoka kwake. Lakini watu ambao kwa kawaida wanataka kwenda na kulipuka kote ulimwenguni na kurarua kabisa, kwa kawaida Mungu hawezi kumtumaini kwa sababu hawezi . . . yeye anataka kulifanya mwenyewe, anaingia katika njia yake mwenyewe nalo. Kama mtu hataki kwenda, basi karibu inambidi Mungu kumsukuma ndani yake, mtu wa aina hiyo ndiye Mungu kwa kawaida humtumia katika Maandiko.

⁵⁷ Nikasema, “Mwishie tu, na kumpenda kwa moyo wako wote, na Yeye atakuweka mahali anapotaka uwe.” Hiyo ni kweli.

⁵⁸ Tunajaribu kuchukua mahali pa mtu mwingine, hatuwezi kufanya hivyo, inatubidi kudumu daima katika wito wetu, ambapo Mungu ametuitia.

⁵⁹ Sasa, tungetaka kusema, ya kwamba kwenye somo hili la Maandiko, usiku wa leo, kwenye mlango wa 17, mtakapoenda nyumbani, nataka msome mlango huo wote.

⁶⁰ Sasa, tunaona ya kwamba Yesu alikuwa akijiandaa kufanya jambo kubwa, kwenye tukio kuu lililokuwa karibu kutukia. Na wakati Mungu anapokaribia kufanya mambo makuu, jambo la kwanza Mungu hufanya kwa kawaida ni kulifanya lijulikane

katika mbingu juu kwanza, Yeye daima hutangaza kazi Zake mbinguni kabla hajazitangaza duniani.

⁶¹ Kama vile wakati wa kuzaliwa kwa Bwana Yesu, ni nani waliokuwa wa kwanza kuja? Ni kitu gani kilichokutangaza kwanza? Nyota ilianza kuenea angani, wale Mamajusi walikuja kote kutoka Mashariki hadi—hadi Yerusalemu kutoka India, wale Mamajusi watatu.

⁶² Nilipokuwa India, ungali unawaona vivyo hivyo, wameketi moja kwa moja mtaani, kile wanachoita wenye hekima, ama Mamajusi, watazama nyota, kama wengine wanavyowaita.

⁶³ Lakini Mungu daima hutangaza mambo mbinguni kabla hajayatangaza duniani. Na hili lilikuwa tukio maalum. Petro, baadaye maishani, aliuita mlima mtakatifu. Sasa, siamini ya kwamba huyo mtume alimaanisha ya kwamba mlima huo ulikuwa mtakatifu, kwa sababu ulikuwa ni mlima tu, vita vilikuwa vimepiganiwa humo, na kadhalika. Haukuwa mlima mtakatifu, bali ilikuwa ni Mungu Mtakatifu juu ya mlima, si mlima mtakatifu.

⁶⁴ Tunasikia mengi sana siku hizi kuhusu kanisa takatifu, ama watu watakatifu, hakuna kanisa takatifu, wala watu watakatifu, ni Roho Mtakatifu ndani ya watu anayefanya utakatifu. Si kanisa takatifu, ama watu watakatifu, ni Roho Mtakatifu kanisani.

⁶⁵ Sasa, kwenye tukio hili, Mungu aliwachagua watatu kutoa ushahidi, Yeye aliwachukua Petro, Yakobo, na Yohana. Na kama ukiangalia, daima, alipoenda kufanya jambo kubwa, aliwachukua hao watatu. Sijui ni kwa nini. Petro, Yakobo, Yohana: tumaini, imani, na upendo, zile karama tatu kuu zaidi za Mungu, tumaini, imani, na upendo. Yohana, bila shaka, akiwa ni upendo alikuwa ni upendano, na Yakobo ni tumaini, na Petro alikuwa imani. Naye akawachukua tumaini, imani, na upendo kutoa. . . kutafuta kujua, ama, kuweka ndani yao, kile alichokuwa anaenda kufanya.

⁶⁶ Sasa, tunaona ya kwamba wakati alipopanda kwenda mahali hapa, ambapo baadaye paliitwa mlima mtakatifu, ama mahali patakatifu ambapo Mungu alikuwa, tunaona ya kwamba huko juu, walipofika mlimani, Mungu alikuwa na watatu kutoka Mbinguni kushuhudia, juu ya mlima alikuwa Musa, na Eliya, na Yesu; kisha hapa duniani kulikuwa na viumbe watatu wa duniani, Petro, Yakobo, na Yohana; pia kulikuwako na Musa, Eliya, na Yesu, mashahidi watatu wa Mbinguni, mashahidi watatu duniani.

⁶⁷ Mungu anapojiandaa kufanya jambo fulani, Yeye daima ana shahidi wa jambo hilo. Nina furaha sana leo kwamba tunaweza kuangalia kote kabla ya Kuja kwa Bwana na kuona mashahidi wa kuonekana Kwake, tukiona zile ishara katika Kanisa za kuonekana kwa Bwana Yesu Kristo, tukiona kukitimia Neno

kwa Neno; hata ishara ya mwisho ambayo ilikuwa itolewe kwa Kanisa kabla ya kuonekana kwa Bwana Yesu, inatenda kazi Kanisani sasa hivi, lile jambo la mwisho.

⁶⁸ Kumbukeni, Yeye alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Angalieni yale wenye dhambi waliyokuwa wakifanya Sodoma, angalieni yale Malaika wa Bwana aliyofanya wakati aliposhuka kuja kushuhudia jambo hilo, angalieni yale wale Malaika watatu waliyofanya, wote watatu. Angalieni ulimwengu siku hizi katika dhambi yake, angalieni kanisa siku hizi katika hali yake kama Lutu, angalieni Kanisa lililoitwa likilazimika kujitahidi kama Ibrahimu alivyofanya. Mwanamume au mwanamke, siku hizi, anayejaribu kumwishia Mungu hana budi kujitahidi apate kuendelea; inakubidi kukaza mwendo kuingia katika Ufalme wa Mungu.

⁶⁹ Loo, inasikitisha, lakini hebu na tuliangalie. Angalieni, kule chini alikuwepo mwenye dhambi, angalieni hiyo dhambi ilikuwa ni nini, wanaume walikuwa wamejitia unajisi sana hata hawakuwa na matumizi ya kawaida kwa mke. Angalieni ulimwengu siku hizi, dhambi nyingi sana zimepenya kanisani na katika taifa hata limejaa dhambi. Hiyo ni kweli.

⁷⁰ Najua hili linasikika la mtindo wa kale, mhudumu mmoja alinipeleka kando, si muda mrefu uliopita, na kusema, “Ndugu Branham, unajua ni kwa nini huduma yako siyo huduma iliyo kuu kuliko zote Marekani leo hii?”

⁷¹ Nami nikasema, “Sijali ikoje Marekani, ninataka kujua ikoje kwenye Vitabu vya Mbinguni, huko juu, ikoje huko.”

⁷² Akasema, “Vema, nitakwambia, ni kwa sababu unawakemea watu sana,” kasema, “u—u—unawakaripia sana, na inawaudhi.” Kasema, “Kama ukiacha tu kufanya hivyo, basi,” akasema, “huduma yako ingekua,” na—na kadhalika.

⁷³ Nikasema, “Bwana, hebu nikwambie jambo fulani, inapofikia mahali ambapo inanibidi kupatana juu ya Neno la Mungu, basi nitasimama na kuondoka hudumani, na kumwacha Mungu amwite mtu mwingine kuifanya.” Unawezaje kutulia? Ukitaka kuwa mwaminifu, kuwa mwaminifu. Niambie mtu katika wakati wowote, niambie... Nikasema, “Uliniita nabii, mimi siiti... ulisema, wewe mwenyewe, hivyo, wewe ndiwe uliyesema hivyo. Ndipo basi kama mimi... Kama Bwana akinitia mafuta kwa ajili ya jambo fulani, ningewezaje kutulia basi? Unawezaje kufanya hivyo? Mtu fulani hana budi kuikemea.” Hiyo ni kweli.

⁷⁴ Mungu anaweza kumwinulia Ibrahimu watoto katika mawe haya. Lakini lazima tuwe waaminifu na kusema ukweli juu yake. Mliona...? Loo, bila shaka, hii huduma Marekani haitendi kazi kama inavyotenda ng'ambo, la hashu, kwa sababu Marekani ni nchi iliyoteketea, imekwisha, imelimwa kabisa huku na huku.

⁷⁵ Yesu alisema Ufalme ni kama kwenda kwa...mtu aliyechukua jarife na kulitupa baharini na kukusanya kutoka kwake, wakati mwingine alikuwa na kamba, alikuwa na nyoka, na mijusi, na vyura, na samaki. Baada ya kitambo kidogo, hupati kitu ila wavu uliojaa mijusi na vyura, samaki wote tayari wameingia.

⁷⁶ Kwa hiyo, tunavua tu mpaka wa mwisho atakapovutwa atoke, ndipo Yesu atakuja. Tunajuaje hao ni akina nani? Unatupa tu jarife la Injili na kulivuta. Hiyo ndiyo sababu nimekuja hapa pamoja na ndugu zangu, kusimama pembeni mahali fulani na kutupa jarife pamoja nao, ninyoshe mkono kwa huduma yangu na kuivuta, niseme, "Hao hapo, ndugu." Ni kitu gani?

⁷⁷ Sasa, lakini hili ni eneo lililotekezwa kabisa. Mliona huko nyuma nilipowajia kwa mara ya kwanza huko Oregon? Watu walikuwa wakija kutoka kila mahali, maelfu mara maelfu wakisongamana. Loo, ilikuwa sawa, nilikuwa tu nikiendelea kuwaombea wagonjwa, lakini niliporudi na kuanza kuielezea ile kweli, kusesitiza Injili, loo, wengi waligeuka.

⁷⁸ Linganisha hilo na siku zilizopita za Bwana wetu. Wakati alipokuwa akiwaponya wagonjwa na wanaoteseka, watu wengi walimjia, alipowalisha elfu tano, watu wengi walikuja. Lakini wakati alipoanza kuketi chini na kuwaambia ukweli, ilikuwaje? Wote wakaanza kugeuka. Yeye...Hata wale sabini waligeuka.

Naye akawaambia wanafunzi, "Je, ninyi pia mtaenda?"

Ndipo Petro akasema maneno hayo makuu aliyosema, "Twende kwa nani?" Mnaona?

⁷⁹ Lakini sasa, hilo halikukomesha miujiza Yake, Yeye aliendelea moja kwa moja. Siku chache baadaye, Yeye—Yeye aliyafumbua macho ya mtu ambayo hata hayakuwa na mboni za macho matunduni. Miujiza yake ikawa mikubwa zaidi lakini umati ukapungua, ndipo umaarufu Wake ukapungua zaidi, mpaka wakamsulubisha msalabani.

⁸⁰ Na kama tuna Roho wa Mungu, itakuwa vivyo hivyo kabisa, kwa sababu Roho wa Mungu ni yeye yule, na watu wanabaki vile vile, hiyo ni kweli.

⁸¹ Sasa, tunaona ya kwamba Yeye alikuwa akiwachukua hawa kushuhudia yale aliyokuwa anaenda kufanya. Bila shaka kuna jambo fulani linaloenda kutukia wakati Mungu anapowaita mashahidi Wake pamoja. Naye...Kile alichokuwa anaenda kufanya kule, kile tunachoita, kilikuwa ni kumweka mwana mahali pake.

⁸² Katika Agano la Kale, tunaona ya kwamba wakati mtu alipokuwa na ufalme mkuu, naye alikuwa na—alikuwa na mwana aliyezaliwa nyumbani mwake, basi mwana huyo, bila shaka, alikuwa mwana mara tu alipozaliwa, lakini hata hivyo

hakuwa na urithi mpaka alipowekwa mahali pake, akafanywa mwana mwenye mamlaka katika familia; wanakuika kufanywa mwana mwenye mamlaka. Sasa, hilo linasikika la kigeni.

⁸³ Lakini sasa, hapa ndipo kanisa la Kipentekoste, nionavyo mimi, lilipoenda kombo, ama lilipokwamia, badala ya kuendelea mbele. Sasa, mimi ni Mpentekoste, pia, na kama sikuwa na Roho Mtakatifu, nisingekuwa nimesimama hapa juu nikiwaambia habari Zake, lakini, na kama sikuwapenda, nisingekuwa nikiwaambia habari Zake.

⁸⁴ Lakini angalieni, wakati—wakati mtoto alipozaliwa, katika nyumba ya kale ya kiothodoksi, vema, baba alikuwa na kazi nyingi za kufanya. Kwa hiyo, yeye...Huyo mwana alikuwa mwana mara tu alipozaliwa.

⁸⁵ Vema, hivyo ndivyo kanisa la Kipentekoste, mara lilipozaliwa, ama kanisa lingine lolote, linapozaliwa katika Ufalme wa Mungu, linakuwa wana na binti za Mungu, lakini tulikomea hapo. Wakati kanisa la Kipentekoste lilipopokea karama ya kunena kwa lugha na kufasiri, walikomea hapo. Hapo si mahali pa kusimamia, hapo ndipo mahali pa kuanzia. Mbona, tuna rasilimali zisizotumiwa, kila mahali. “Mambo yote yanawezekana kwao waaminio.” Kila ahadi katika Biblia ni yetu.

⁸⁶ Shida yake ni kwamba, tunaweza kuwaandea raia we—wenzetu wa Ufalme wa Mungu, ndugu zetu Wamethodisti na Wabaptisti, unaweza kuwaambia kuhusu uponyaji wa Kiungu, nguvu za Mungu, watarejea kwenye, “Moody alisema nini juu yake? Mtu mwingine alisema nini juu yake?” wakiangalia nyuma.

⁸⁷ Tunaweza kuwaambia ndugu wa Kipentekoste, “Vema, kile tulicho nacho huko nyuma wakati babu zetu walipokipata miaka hamsini iliyopita,” kamwe usiangalie nyuma, angalia mbele, endelea kuangalia mbele. Sayansi haifanyi hivyo. Sayansi itampata Mungu kabla ya mhubiri kumpata tusipokuwa waangalifu, katika utafiti wake. Hiyo ni kweli.

⁸⁸ Sasa, sayansi, yapata miaka mia tatu iliyopita mwanasayansi Mfaransa alisema, akalithibitisha kwa kuvingirisha mpira, kama dunia, na kusema, “Kama mtu,” akalithibitisha kisayansi, “kama mtu angeweza kwenda mwendo wa kasi sana wa maili thelathini na tano kwa saa, uvutano ungemwondoa duniani.”

⁸⁹ Sasa, mnafikiri sayansi ya kisasa ingesikiliza hilo? La hashu, yeye anaenda maili elfu mbili kwa saa sasa, naye hata hakomei hapo, anaendelea; nasi tunajaribu kuangalia nyuma kuona yale mtu mwingine aliyosema.

⁹⁰ “Mambo yote yanawezekana kwa hao waaminio.” Tuna rasilimali za Mungu zisizotumiwa mikononi mwetu ku—kumwonyesha Mungu. Sisi ni wana na binti za Mungu.

Mungu alimfanya mwanadamu, akamfanya mungu mdogo, akampa mamlaka juu ya nchi, lakini hali yake ya kuanguka ilisambaratisha hayo. Lakini walichopoteza kwa Adamu, kilirudishwa na Kristo.

⁹¹ Yeye alisema, “Ukiuambia mlima huu, ‘Ng’oka,’ wala usione shaka moyoni mwako, bali uamini ya kwamba yale uliyosema yatatimia, yatakuwa yako. Mambo yote, yoyote mtakayo, mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu.” Amina. Alitrudishia yote yaliyopotea katika Adamu.

⁹² Lakini siku hizi, tunafikiri tu kwenda kanisani, kuandika jina letu kwenye kitabu, kutumbukizwa majini ama kunyunyiziwa, ama chochote kile, kupeana mikono na kusanyiko, pamoja na mchungaji, hilo latosha. Ndipo tukafikia Pentekoste, tukampokea Roho Mtakatifu, akatushukia, nasi tukaanza kupaza sauti na kumsifu Mungu, kisha Nguvu za Mungu zikashuka, nasi tukanena kwa lugha, tukawasikia wakiifasiri, wakitoa nukuu kubwa, na kadhalika, na utabiri. Hilo linasikika ni sawa, bali tunakoma tu, huo ni mwanzo tu, endelea tu kusonga mbele, zaidi, na zaidi, na zaidi, Mungu anatutegemea sisi.

⁹³ Wakati mwana huyu alipozaliwa nyumbani, kimahali alikuwa ni mwana, mwana wa baba. Lakini sasa, baba huyo alifanya nini? Hakuwa na wakati wa kukaa na mwana huyo mmoja, biashara yake ilikuwa kubwa, kwa hiyo aliajiri mwalimu au mlezi, mwalimu. Naye alitafuta nchini mpaka akampata mtu anayefaa, kwa sababu huyo alikuwa ni mtoto wake, naye alitaka mtoto huyo alelewe vizuri, kwa sababu mtoto huyo angerithi kila kitu alichokuwa nacho siku moja. Lakini, aliangalia kila mahali, mpaka angeweza kupata mtu anayefaa, si mmoja wa watu hawa wanaojaribu kupata kitu cha kujivunia, aseme uongo, ama, “Loo mtoto wako anaendelea vizuri,” wakati hakuwa anaendelea vizuri. Naye ingembidi kuripoti maendeleo ya huyo mtoto. Sasa, huko kulikuwa ni kufanywa mwana mwenye mamlaka.

⁹⁴ Wahudumu hapa wanaelewa na wanajua ninachozungumzia, kule kufanywa mwana mwenye mamlaka, Paulo katika—katika—katika Wagalatia, na kadhalika, kuwekwa mwana mahali pake, Agano la Kale.

⁹⁵ Nafikiri la King James lilikuwa na wazo hilo, wale wafasiri, aliposema, “Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi.” Nyumba ilikuwa ufalme. Na nyumbani mwa baba, kama vile katika Agano la Kale, nyumbani mwa baba, alikuwa na watumishi wengi, naye akaenda kwa watumishi hawa, hakuwa na wakati wa kumfundisha mwanawe, kwa hiyo akampata mtu mwingine wa kumfundisha kwa niaba yake, mtu afaaye.

⁹⁶ Na hivyo ndivyo Mungu alivyokuwa akituonyesha hapa kwenye kile tunachoita Mlima wa Kugeuka Sura, kile

alichokuwa akifanya Mwenyewe. Mungu kamwe hakumwagiza mtu kufanya jambo lolote ambalo Yeye Mwenyewe asingelifanya, kumbukeni hilo. Mungu asingekuomba ufanye lolote, isipokuwa Yeye Mwenyewe alilifanya.

⁹⁷ Kwa hiyo angalieni, sasa, wakati mwana huyu alipokuwa, alipoanza kufikia umri wa kwenda shule, mwalimu huyu angeambatana na mwana huyu, na kukaa pamoja naye, na kumletea baba ujumbe jinsi huyo mwana alivyokuwa anaendelea. Kama mwana alikuwa m—m—mzembe, hafanyi kazi za baba, basi jinsi ambavyo mwalimu huyo hana budi kuona aibu kwenda mbele ya baba yake, na kusema, “Bwana, ninasikitika kusema, lakini mwa—mwanao hafanyi vizuri sana. Yeye—yeye hataninii, hatajifunza, hajali.”

⁹⁸ Vema basi, Mungu, alipoondoka duniani hapa, Kanisa Lake, Yeye alilichagulia Kanisa Lake Mwalimu, alipata Mlezi, Mtu Ambaye angekuwa mwaminifu, Ambaye angekuwa mkweli, Mlezi anayefaa. Haikuwa ni askofu fulani mkuu, ama papa, ama mwangalizi mkuu, alimtuma Roho Mtakatifu kuwa Mwangalizi na Mwalimu wa Kanisa. Lakini tuliwachukua maaskofu na kadhalika kuwa walimu wa Kanisa, si mpango wa Mungu. Roho Mtakatifu ndiye Mwalimu wetu, Roho Mtakatifu ndiye Mwalimu wa Kanisa.

⁹⁹ Tumechukua wazo la kila namna, shule za kila namna na theolojia, na kadhalika, wakati Roho Mtakatifu anapaswa kuwa akituongoza. Sasa, hiyo ndiyo sababu kanisa liko katika hali liliyomo usiku wa leo, ni kuongozwa na mwanadamu wala si kuongozwa na Roho. “Wana na binti za Mungu wanaongozwa na Roho wa Mungu.” Roho wa Mungu anapaswa kuliongoza Kanisa. Sasa, watu wanaweza kusema lolote, bali Roho Mtakatifu atasema kweli juu yako.

¹⁰⁰ Sasa, usiku wa leo, unafikiri Roho Mtakatifu hapana shaka anajisikia namna gani inapombidi kuja mbele za Baba na kusema, “Baba, loo, kanisa Lako! Hmm! Unajua nini? Kanisa Lako, nusu yao hata hawaji kanisani Jumapili, la. Jumatano usiku, wanakaa nyumbani kuangalia *Tunampenda Susie*,” ama chochote kile kwenye televisheni, mwajua. “Wanapenda mambo ya ulimwengu kuliko wanavyopenda sifa na nguvu za Mungu”? Hiyo ni kweli.

¹⁰¹ Sina kitu dhidi ya televisheni, kuna mambo mazuri mle, lakini wakati Mkristo atakapokaa nyumbani asiende kanisani kuona mchezo wa kijinga namna hiyo, kuna jambo fulani lililotukia katika maisha ya mtu huyo. Roho Mtakatifu ametoka akaenda mahali fulani, hufanyi kazi ya Baba.

¹⁰² Unafikiri Yeye anafanya nini anapokuja mbele za Baba na kulazimika kusema ya kwamba binti Zake, watoto Wake, binti Zake wapendwa wanavaa nguo hizi za kizinifu, wanazoziiita kaptura? Binti zake!

¹⁰³ Nilisema hilo si muda mrefu uliopita, ndipo mwanamke fulani akaniambia, akasema, “Sikiliza, ngoja, Ndugu Branham,” alikutana nami nyuma ya jengo, akasema, “sikiliza, Ndugu Branham, mimi sivai kaptura.”

“Vema,” nikasema, “hilo ni zuri sana.”

Akasema, “Mimi huvaa suruali ndefu.”

Nikasema, “Hizo ni mbaya zaidi.” Hiyo ni kweli.

¹⁰⁴ Biblia ilisema ni chukizo kwa mwanamke kuvaa vazi limpasalo mwanamume. Mungu habadiliki. Alimfanya mwanamume aonekane kama mwanamume, na mwanamke aonekane kama mwanamke, lakini siku hizi wanaume wamekuwa dondoadume sana, hawajui jinsi ya kuvaa. Hiyo ni kweli. Nao wanawake, binti za Mungu, wakivuta sigara, hujuma kubwa kuliko zote ulimwengu uliyopata kuwa nayo.

¹⁰⁵ Sihofii Urusi kuiangamiza Marekani, Marekani inajiangamiza yenyewe. Robini anayelidonoa tofaa siye anayelidhuru, ni yule mdudu kwenye kiini, anayeliua hilo tofaa. Hiyo ndiyo shida ya makanisa na hili taifa siku hizi, ni dhambi iliyo kwenye kiini, mbali na Mungu.

¹⁰⁶ Mama fulani aliniambia, akasema, “Ndugu Branham, hawatengenezi nguo zingine, inatubidi kuvaa nguo za aina hiyo.”

¹⁰⁷ Dada, wangali wanatengeneza vitambaa, na wanatengeneza cherehani, hakuna udhuru kwake hata kidogo.

¹⁰⁸ Kuna nini? Ni pepo mchafu aliyewaingia. Ilikuwa haramu kwa wanawake wetu wa Kipentekoste kukata nywele zao. Sasa, uligusa kitu fulani, sivyo? Nini kilitukia? Baadhi yao walikuwa wakisema wanaumwa na kichwa, kuumwa sana na kichwa.

¹⁰⁹ Unajua, Biblia ilisema mwanamke akikata nywele zake, anamwaibisha mumewe; mwanamke asiye na heshima si haki kuishi naye. Simaanishi wewe ni katili, lakini ninamaanisha ya kwamba ibilisi na baadhi ya mimbara dondoadume, ambaye anapaswa kuwa huko nje kama mfuga nguruwe badala ya mhubiri, anapaswa kutoka nje na kusema ukweli juu yake, ili mpate kujua ukweli ni upi. Hiyo ni kweli, ndugu?

¹¹⁰ Nilikuwa na rafiki mzee Mmethodisti aliyekuwa akiimba wimbo:

Tulilegeza kamba, tulilegeza kamba,
Tulipatana na dhambi.
Tulilegeza kamba, kondoo wakatoka nje,
Lakini mbuzi waliingiaje?

¹¹¹ Mnaona? Shida ni nini? Walilegeza kamba, mazoea ya kawaida ya mtindo wa kale ya Roho Mtakatifu ambaye huliongoza Kanisa na kulielekeza katika kweli yote. Sasa, hiyo ni kweli, hiyo huenda ikawa ni ya mtindo wa kale, huenda ikaumiza kidogo.

¹¹² Mwajua, nilipokuwa mvulana mdogo, kuna jambo moja ambalo siwezi kulivumilia bado, ni mafuta ya mbarika, Na—naweza tu kunusa harufu yake, nami nitakuwa mgonjwa kwa juma zima, tulipokuwa watoto wadogo, ilimlazimu Mama kushuka kwenda kule ambako wangeninii...dukani, duka la nyama, anunue ngozi za nyama. Naye angezichemsha, ama, azibanike kwenye sufuria kuukuu, na kupata grisi ya kuokea ke—keki za mahindi, ndivyo tulivyoziita, keki za mahindi, nasi tungekuwa na mbaazi macho meusi, mboga za tanipu, nacho kilikuwa ni chakula kizuri sana.

¹¹³ Na, lakini tulipokuwa tu na chakula hicho cha mchana, kiamshakinywa, na chakula cha jioni, basi...Tungeninii, kila Jumamosi usiku, sisi sote watoto wadogo ingetubidi kuoga. Ninakumbuka Mama alipotuingiza ndani, alikuwa na beseni kubwa ya mwerezi. Nao wangeanza na mtoto mchanga, alioga kwanza, nasi tulikuwa kumi, nikawa wa mwisho, maji yale yale, kuongeza tu kidogo zaidi, kuyapasha moto. Halafu basi, sisi watoto shuleni ilitubidi kunywa dozi ya mafuta ya mbarika.

Loo, wakati wangu ulipowadia, ningeshika pua yangu, ningesema, “Mama, Mama, tafadhali usifanye hivyo. Loo, yana—yananichefua sana.”

Ninamkumbuka maskini huyo mama yangu wa kusini, angesema, “Lakini angalia, Billy, kama hayakuchefui, hayakufai kitu.”

¹¹⁴ Na hivyo ndivyo ninavyoihubiri Injili, kama hii ikikuchefua, huenda ikachochea baadhi ya maakuli yako ya Biblia na kuanzisha mambo. Sawa. Hiyo ni kweli. Tunahitaji Injili ya mtindo wa kale, tunahitaji nguvu za Mungu, Roho Mtakatifu arudi ndani, na nyota wote wa Hollywood na televisheni waondolewe.

¹¹⁵ Unajua, mama, ninataka kukwambia jambo fulani, nitawaendea wanaume, kwa dakika moja tu, lakini, mama, ninataka kukwambia jambo fulani. Je, ulijua huyo ni pepo mchafu aliyekuja juu yako? Je, unajua maskini mama anayeshuka mtaani amevalia kizinifu kabisa, unajua ya kwamba mwanamke huyo atawajibika kwa kufanya uzinzi? Mbona, huenda akawa safi kama yungiyungi kwa mpenzi wake wa kiume, ama kwa mumewe, lakini Biblia ilisema, Yesu alisema, “Kama...Kila mtu amtazamaye mwanamke kwa kumtamani amekwisha kuzini naye moyoni mwake.”

¹¹⁶ Halafu basi, kama ukivalia namna hiyo, na mwenye dhambi fulani akuangalie namna hiyo, kwenye Siku ya Hukumu atakapowajibika kwa kufanya uzinzi, itakuwa ni pamoja nawe, na itakuwa ni kosa lako, kwa sababu ulijianika kwake. Huenda usirudi kesho usiku, lakini utasikia wakati mmoja. Unaona? Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Ni pepo mchafu, mwovu.

¹¹⁷ Nawe unafikiri Roho Mtakatifu anawazia nini anapokuja mbele za Baba kusema ya kwamba watoto Wake wanatenda hivyo?

¹¹⁸ Miaka mingi iliyopita, huko chini ku—kusini wakati walipokuwa wakiwachukua watu weusi na kuwauza kama watumwa (Hilo kamwe halijawahi kuwa sahihi. La, bwana. Mungu—Mungu alimfanya mwanadamu, mwanadamu akawafanya watumwa.), nao walikuwa wakija na kuwanunua maskini watu hao kama tu vile ungefanya hapa nje kwenye eneo la magari ya mitumba, wanachukua tu hati ya mauzo na kuwauza. Kulikuwa na madalali waliokuja na kuwaona watu hao, nao wangewachukua hao wanaume wakubwa mno, wanene kutoka kwa wake zao, na kuwazalisha na mwa—mwanamke mkubwa zaidi, ama chochote kile, kuleta kundi bora zaidi la watumwa.

¹¹⁹ Namkumbuka Abraham Lincoln wakati alipovua kofia yake na kuigongesha mikono yake namna hiyo, kasema, “Hilo ni kosa na siku moja nitalipiga.” Mungu atupe rais kama Abraham Lincoln tena. Naam. Aliposema hivyo, alikuwa sahihi.

¹²⁰ Ninakumbuka wakati fulani uliopita, hapa Illinois, nilikuwa kwenye jumba la makumbusho, nami nikamwona mzee, mtu mweusi akienda pale, maskini mzingo wa nywele nyuma ya kichwa chake. Alikuwa akipitia kwenye jumba la makumbusho akiangalia, na baada ya kitambo kidogo, akasimama, naye akaangalia, akainama nyuma, akaanza kulia, huku machozi yakitiririka usoni mwake, alikuwa anaomba. Nikamwangalia kwa dakika chache, nikamkaribia, nikasema, “Hujambo, Mjomba?”

Naye akasema, “Sijambo?”

Nami nikasema, “Mimi ni mhudumu.” Nikasema, “Ningetaka tu kujua ni kwa nini ulikuwa unaomba. Ni kitu gani kilichokusisimua?”

Kasema, “Njoo hapa.”

¹²¹ Nikaangalia mle ndani kwa darubini ndogo, na hapo kulikuwa na nguo, nikasema, “Ni nguo. Sioni chochote cha kufadhaisha sana hapo, isingemfanya mtu aruke nyuma na kuomba dua.”

¹²² Akasema, “Lakini angalia, ningali nina alama za mshipi wa utumwa mwilini mwangu,” akasema, “na hiyo ni damu ya Abraham Lincoln, nayo damu ya Abraham Lincoln iliniondolea ule mshipi wa utumwa mwilini mwangi. Si ingekusisimua, pia?”

¹²³ Nikasimama nyuma, nami nikasema, “Kama damu ya Abraham Lincoln ingemsisimua mtumwa kwa kuondolewa mshipi, Damu ya Yesu Kristo inapaswa kufanya nini wakati inapohubiriwa kwa nguvu zake mbele ya kanisa linalodai kuzaliwa mara ya pili! Inapaswa kufanya nini?”

¹²⁴ Siku moja wakati wao...[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] ...nao wangechukua mijeledi na kuwacharaza kuwafanya—kuwafanya wafanye kazi. Nao wakamwona kijana mmoja katika shamba fulani hili, haikuwalazimu kumcharaza, ndugu, alikuwa kifua mbele, kidevu juu, alikuwa tayari kabisa.

Ndipo dalali huyu akasema, “Ningetaka kumnunua mtumwa yule.”

“Loo, lakini,” mwenye mali akasema, “hauzwi.”

Akasema, “Vema, yeye ni tofauti sana na hao wengine.”

Kasema, “Naam, nimetambua hilo.”

“Vema,” kasema, “Nadhani yeye ndiye bosu juu yao wote.”

Kasema, “La, yeye ni mtumwa tu.”

Akasema, “Vema, labda unamlisha vizuri kuliko unavyowalisha hao wengine.”

Akasema, “La, wote hula huko nje kwenye manchani pamoja.”

Akasema, “Vema, ni kitu gani kinachomfanya tofauti sana na vile hao wengine walivyo?”

¹²⁵ Ndipo mwenye mali akasema, “Hilo lilinishangaza kwa muda mrefu, pia. Lakini nilikuja kugundua, huko katika nchi ya uenyeji wake anakotoka, baba yake ndiye mfalme wa hilo kabila. Na ingawa, yeye ni mgeni katika nchi nyingine hapa, mbali na nyumbani, bali anajua yeye ni mwana wa mfalme, naye anaenenda kama mmoja.”

¹²⁶ Ndugu, dada, kama Mwafrika katika nchi ya kigeni angeweza kuenenda, akitenda kama mwana wa mfalme, hivi haitupasi kama wana na binti za Mungu kutenda hivyo, na kujiendesha kama wana na binti za Mungu, wakati Baba yetu ndiye Mfalme? Basi wanawake wanapaswa kuvaa kama binti za Mungu. Hiyo ni kweli.

¹²⁷ Nao wanaume, loo, jamani, mwanamume yeyote atakayemruhusu mkewe kuvaa kaptura na kuvuta sigara, nina maoni duni kuwa yeye ni mwanamume. Hiyo ni kweli. Anapaswa kuwa ndiye kiongozi wa nyumba, inaonyesha ni nani bosu huko. Hiyo ni kweli kabisa. Naam, loo, mimi. . .

¹²⁸ *Mwanamume* hapimwi kwa misuli, huyo ni mnyama, *mwanamume* hupimwa kwa tabia. Nimeona watu waliokuwa na uzito wa ratili mia mbili, na misuli yote, ila hawakuwa na hata chembe moja ya mwanamume ndani yake, wakimtupa mtoto mchanga kutoka mikononi mwa mama na kumnajisi. Huyo si mwanadamu, huyo ni mnyama, huyo ni mnyama, *mwanamume* ni tabia.

¹²⁹ Hapajawahi kuwapo na mtu kama Yesu Kristo, bali Biblia ilisema hakuna uzuri hata tumtamani. Labda ni Jamaa mdogo, aliyeinama begani, ama chochote kile, “sote tulimficha

nyuso zetu.” Lakini Yeye. . . Hakujuwahi kuwa na tabia kama hiyo, hivyo ndivyo *mwanamume* halisi alivyo. Huipimi misuli ya mwanamume, bali kwa sugu za magoti katika suruali yake ambapo amekuwa akiomba, hivyo ndivyo unavyompima mwanamume, kwa tabia. Ni kweli.

¹³⁰ Loo, jinsi ambavyo Roho Mtakatifu hana budi kuona haya kuja mbele za Baba akisema, “Unajua nini? Watumishi Wako wanapatana, wanaanza kusema, ‘Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu. Wala hatuhitaji kupiga makelele huko kwote, na kunena kwa lugha, na karama, hebu tuwe tu kanisa.’ Wakaondoa utukufu wote kutoka kwa nguvu kanisani, na labda wakaugauza ukawa namna fulani ya dhehebu.”

¹³¹ Hilo ni sawa, bali mradi tu dhehebu linadumu na nguvu za Mungu, Mungu abariki dhehebu hilo. Hiyo ndiyo sababu mimi ni Mpentekoste leo, kwa sababu nafikiri lina nguvu zaidi za Mungu ndani yake kuliko shirika lolote nililopata kuona. Lakini wakati nguvu za Kipentekoste zitakapoondoka kwenye kanisa la Kipentekoste, nitaambatana nazo. Hiyo ni kweli, bila shaka. Dumu na Mungu.

¹³² Wakati Waisraeli walipofuata, waliifuata Nguzo ya Moto, kila iliposimama, wakapiga kambi moja kwa moja chini Yake. Martin Luther alikuwa ndiye wa kwanza kuona ule Moto ukiondoka kwenye kanisa la Kirumi, naye akaambatana na huo Moto chini ya kuhesabiwa haki, “Mwenye haki ataishi kwa imani.” Alijiundia dhehebu lake, akaandika ninii yake, kanuni zake zote za imani na kuzitia nukta, kituo kikuu, “Hii ndiyo yote. Tunaamini hili kama Walutheri.” Muda si muda mwajua, ile Nguzo ya Moto ikaanza kuondoka, Luther asingeweza kuendana nayo. Kwa nini? Kwa sababu tayari ana kanuni zake za imani zimewekwa, kanisa lake limejiundia dhehebu, kila kitu kiko karibu nalo.

¹³³ John Wesley aliuona, utakaso, kazi ya pili ya neema, naye akaondoka akaifuata. Naye akauteketeza ulimwengu, akaleta kuhesabiwa haki Uingereza, Marekani, watu wote wakuu. Moja ya miamsho mikubwa sana tuliyopata kuwa nayo ilikuwa ni uamsho wa Wesley, umehesabiwa miongoni mwa iliyo mikuu sana tuliyopata kuwa nayo. Lakini walifanya nini baada ya kupata utakaso? Walijenga madhehebu yao chini yake, wakachukua kalamu ndogo, “Sisi Wamethodisti tunaamini *hili*, na *hili*, na *hili*, na *hili*,” na kumalizia fundisho lao kwa kituo kikuu. “Hilo ndilo tunaloamini.”

¹³⁴ Malaika wa Bwana akaondoka, mbona, Wamethodisti wasingeweza kuambatana Naye, nao Wapentekoste wakaiona. Ubatizo wa Roho Mtakatifu, kurudishwa kwa karama, hao wakaenda, upesi tu walivyoweza kwenda, wakawaacha Wamethodisti moja kwa moja kivulini, Wapilgrim Holiness,

Wanazarayo, na hao ambao hawangeendelea, wakaendelea moja kwa moja Nalo. Na wakati ninii . . . Muda si muda mwajua, sasa imekuwaje kwa Pentekoste? Wamejijengea klabu ndogo.

¹³⁵ Lakini Nguzo ya Moto itaondoka moja kwa moja, hebu tuifuata, tuchukue makanisa yetu, tuchukue ndugu zetu, hebu tuchukue Lutheri, Baptisti, Methodisti. Pentekoste, nimesema, si dhehebu, Pentekoste ni tukio. Nilikuwa Mbaptisti na nikapata baraka za Kipentekoste. Kuna Methodisti, Lutheri, na wa kila namna hapa wanaompokea Roho Mtakatifu, Wakatoliki, Wayahudi, makafiri, chochote kitakachokuja na kumwamini Bwana Yesu Kristo na kumkubali katika utimilifu wa nguvu Zake. Yeye ndiye Mwalimu wa Kanisa, Yeye Ndiye. Acha Roho Mtakatifu aishi kanisani na kufanya njia, hapo ndipo mtakapokuwa na mikutano halisi.

¹³⁶ Msikilizeni mchungaji wenu, asije, hebu. . . Mnaona, kama ibilisi hawezi kukuzuia kuona kitu kilicho halisi—halisi cha Mungu, atakusukuma mbali sana hata ukiuke mipaka nacho, namna hiyo, atakufanya uingie kwenye ulokole. Si lazima uwe na ulokole, kuna mambo mengi sana yaliyo halisi na ya kweli sio lazima uwe mlokole, jamani, anga zote za Kipentekoste zimejaa hayo.

¹³⁷ Lakini msikilizeni mchungaji wenu, mtu mzuri, aliyetumwa na Mungu, mwalimu atakayetuma na kuwaambia la kufanya hasa, kwa sababu yeye mwenyewe ametiwa mafuta na Roho Mtakatifu. Basi mwangalieni, yeye atadumu moja kwa moja na Neno, yale hasa Neno lisemayo, atalisema moja kwa moja pamoja Nalo. Naye Mungu atalibariki Neno hilo, sijali liko wapi, Yeye atalibariki kwa sababu aliahidi angefanya hivyo. Hiyo ni kweli. Atadumu.

¹³⁸ Wewe dumu moja kwa moja kwenye Neno, na Neno hilo ni Uzima. Na kila unapolipokea Neno, unapokea Uzima. Liingize moyoni mwako na uliamini Hilo kama mali yako mwenyewe, kila ahadi ni yako. Mungu alikupa kitabu cha hundi, ulipompokea Roho Mtakatifu huku Jina la Yesu limeandikwa chini ya, kwa chochote utakacho. Unaogopa kuijaza? “Ombeni mtakalo katika Jina Langu, Mungu atawapa.” Ninapenda hilo. Loo, jamani, simameni hapo kwa imani isiyoghoshiwa. Ombeni na kuamini, na itatimia; hiyo ndiyo njia ya kulifanya.

¹³⁹ Sasa, wakati baba angetembea mbele, ama, mwalimu angeenda mbele za baba. . . Sasa, kumbukeni, hatampata jamaa fulani, ambaye atajaribu tu kujipendekeza, na kujitetea, na, “Vema, nitakwambia, yeye ni jamaa mzuri, yeye ni mtoaji mzuri kanisani, wala hatuwezi kumtoa kwenye halmashauri ya mashemasi, ingawa ameo mara tatu nne, lakini kamwe hatuwezi kufanya hivyo, kwa sababu tukifanya hivyo, yeye ndiye tegemeo kuu kwa kanisa.” Yeye ni kizuizi kwa kanisa, kabisa.

¹⁴⁰ Tunachohitaji leo ni kanisa halisi, la kweli, lililosafishwa, lililojazwa na Roho Mtakatifu, limejaa Roho Mtakatifu, tayari, limejazwa, na kupakwa mafuta na Roho Mtakatifu wa Mungu. Naam, bwana. Ninaamini ya kwamba ninii... Tukishindwa kulihubiri, Mungu atawainua Wabaptisti, ama Wapresbiteri, ama mtu fulani wa kufanya hivyo. Hakika atafanya hivyo, maana atakuwa na Kanisa kule lisilo na waa wala kunyanzi, atafanya hivyo.

¹⁴¹ Kwa hiyo, ndugu, hebu na tujitikise tu, na tuinuke kutoka mavumbini, na kujitikisa, na kuingia kwenye njia kuu ya Injili ya kale, na kupanda kwenye barabara kuu. Hilo ndilo jambo pekee la kufanya ni, “Twendeni mbele, enyi askari wa Kikristo.” Hakuna wakati wa kulegea, ama kuwa rahisi sasa, hima tuanze kuuendea Ufalme wa Mungu.

¹⁴² Sasa, sasa tunaona basi, vipi kama mvulana huyu alikuwa ni mvulana mzuri? Loo, jinsi ambavyo hapana shaka yule Mwalimu alifurahia kwenda mbele za Baba, na kusema, “Baba, nina furaha sana kukwambia! Unajua, huyo mvulana Wako ni kama tu ulivyo Wewe. Unajua, yeye atasoma Neno Lako, naye atasema, ‘Hiyo ni kweli kabisa, hivyo ndivyo Baba yangu alivyosema. Baba yangu hawezi kusema uongo, ninaliamini jinsi tu Yeye alivyolisema.’”

Loo, jinsi ambavyo Baba hana budi kusema, “Huyo ni—huyo ni mvulana Wangu!” Mnaona? Sasa, hivyo ndivyo Mungu anavyotaka kutufanyia.

¹⁴³ Sasa, sasa, kama mvulana huyo alizaliwa, sasa sikilizeni, kama mvulana huyo alizaliwa nyumbani kama mwana, bali hakuwa mvulana m—mwema, asingefuata maagizo ya baba yake, asingekuwa kazini mwa baba yake, mvulana huyo daima alikuwa ni mwana, lakini kamwe hakuwa na urithi wowote. Mlijua hilo? Kamwe hakupata urithi wowote, alikuwa ni mtu aliyetupwa tu; daima alikuwa mwana.

¹⁴⁴ Basi unapompokea Roho Mtakatifu, wewe ni mwana wa Mungu ama binti wa Mungu, hiyo ni kweli vya kutosha, bali usipomtii Mungu, utembe katika Nuru, utembe katika Neno, umwamini Mungu, basi hutakuwa na urithi wowote. Vema, hivyo ndivyo hasa Mungu anavyofanya bado.

¹⁴⁵ Sasa angalieni hili, sasa, vipi kama huyo mvulana alikuwa ni muungwana mwenye haki? Alimpenda tu baba yake, alipenda kuwa katika shughuli za baba yake. Alipenda kuona mashamba yote ya mizabibu yamelimwa vizuri kabisa, kila mtu kwenye mahali pake pa wajibu. Naye akamwona mtu akikwepa, akamwendea, na kumkumbatia, kasema... “Hivi majuzi, mbona, baba, alienda kule, naye akaona mtu huyu alikuwa anakwepa kazi, kwa hiyo akaenda pale na kuweka mkono wake begani mwake, na kusema, ‘Bwana, wewe ni

mtumishi wa baba yangu. Unaona?" Na kuanza . . . Kama tu vile ungalifanya."

¹⁴⁶ Loo, baba aseme, "Unajua, kweli ninampenda mvulana huyo, huyo ni mwanangu." Kama tunavyoliita huku Marekani, "amemshabihi kabisa babaye," mwajua. "Yeye—yeye—yeye ni mvulana wangu, ninamjivunia."

¹⁴⁷ Mnajua kilichotukia basi wakati mvulana huyo alipokuwa na umri fulani? Mvulana huyo alipewa mamlaka katika hiyo familia. Sasa, walifanya nini? Walimpeleka nje hadharani, wakamvika joho maalum, kisha wakafanya sherehe. Ndipo watu wote wa miji wakakusanyika na kutazama, kisha wakamwambia mvulana huyo, ndipo baba akafanya sherehe ya kufanywa mwana mwenye mamlaka. Baada ya . . . Loo, msikose hili! Baada ya mwana huyo kupewa mamlaka, jina lake kwenye kitabu cha hundi lilikuwa sawa tu na la baba yake.

¹⁴⁸ Hapo ndipo Mungu anapojaribu kulifikisha Kanisa Lake. "Uambie tu mlima huu, 'Ng'oka,' nao utang'oka." Mamlaka, wana wa Mungu! Viumbe vyote vinaugua, vikingojea kudhihirishwa kwa wana wa Mungu, wakingojea mahali ambapo ugonjwa huo utakuwa, "Simama!" na itakuwa hivyo. Vipofu wataona. Viziwi na bubu, tunawaombea sasa, lakini wakati huo mtaumuru. Haikusema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, watawaombea wagonjwa." Yeye alisema, "Watatoa pepo." Sio, "Nitawatoa." "Watawatoa."

¹⁴⁹ "*Ukiuambia* mlima huu." Sio, "Kama nikiuambia." "*Ukiuambia* mlima huu, 'Ng'oka,' usitie shaka moyoni mwako." Tunachohitaji ni kufanywa wana wenye mamlaka, wana na binti wanahitaji kupewa mamlaka.

¹⁵⁰ Lakini kanisa linawezaje, kanisa la Kipentekoste, na makanisa ya Kimethodisti, na ya Kibaptisti kupewa mamlaka mpaka watakaposhika nidhamu? Hatuna budi kuwa na nidhamu kwanza, Mungu asingeweza kuaminisha nguvu hizi kwa kanisa, ni vigumu kujua mngefanya nini.

¹⁵¹ Baba angewezaje kuaminisha biashara ya—yake kwa mvulana ambaye huenda akauchafua kirahisi tu urithi wake wote? Asingeweza kufanya hivyo. Kanisa halina budi kufikia mahali ambapo limeadabishwa. Mungu yuko kwenye kazi hiyo sasa hivi, nidhamu.

¹⁵² Sasa, alimpeleka huyo mwana nje, naye akafanya sherehe, ndipo akasema, "Huyu ni mwanangu, nami ninamfanya mwana mwenye mamlaka katika familia yangu, lolote asemalo, ninalisema, pia."

¹⁵³ Sasa, Mungu alikuwa akimfanyia Yesu jambo lile lile pale, alikuwa akifanya yale hasa aliyowataka wafanye. Yeye, Yesu alikuwa amempendeza, ndipo akampandisha juu, na kuchukua mashahidi watatu wa duniani, Petro, Yakobo, na Yohana (tumaini, imani, na upendo), akamshusha Musa na Eliya chini

kushuhudia huku kufanywa mwana mwenye mamlaka kukuu. Naye alifanya nini? Biblia ilisema ya kwamba Yeye aligeuka sura, “Na mavazi Yake yakametameta kama jua,” vazi maalum. Amina. Hmm! Vazi maalum, upako maalum. Nao walipotazama juu, walimwona akiangaza katika utukufu wa Mungu, ndipo Sauti ikasema, “Huyu ni Mwanangu mpendwa, msikieni Yeye.” Loo, jamani!

¹⁵⁴ Kile Mungu anachotaka kufanya na Kanisa usiku wa leo, anachotaka kufanya na mtu binafsi, ni kumpata mtu fulani, kutafuta, Roho Mtakatifu anatafuta watu, anayeweza kumpeleka mahali fulani, azungumze na mtu huyo, awatie mafuta, na kuwapa kitu maalum, nguvu kuu na karama kufanya mapenzi Yake na kutekeleza mapenzi Yake.

¹⁵⁵ Lakini anawezaje kufanya jambo hilo wakati inambidi daima kujitokeza, aseme, “Loo, ni mbaya sana! Ndio—ndio kwanza—wa—wakimbilie tu *hili*. Wamekimbilia kosa. Ha—hawataenda kanisani. Wao—wao—wao...Ni...” Angalia ha—hali kanisa liliyomo. Kwa hiyo, kama Mungu hawezi kuufanyia mwili, Yeye atawachagua watu binafsi na kulitekeleza. Mungu anaweza kutoka kwenye haya mawe kumwinulia Ibrahimu watoto.

¹⁵⁶ Angalieni, mara tu tukio hilo la ghafla la kimbinguni lilipotukia, Petro alifanana sana na ulimwengu siku hizi, mara tu mambo ya kimbinguni yalipofanyika, mwujiza mkuu ulifanywa... Vema, kama tu katika siku za Musa, kulikuwako na umati uliochanganyikana.

¹⁵⁷ Musa alishuka akaenda Misri. Basi aliposhuka kwenda kule, ilikuwaje? Alifanya miujiza kadhaa, na alipoifanya, mwaminio na asiyeamini wote wakakusanyika, kwa sababu miujiza huwasisimua watu. Basi kulikuwako na umati wa watu waliochanganyikana walioambatana nao, ndipo kundi lilo hilo lililochanganyikana likaichafua kambi. Loo! Si kujaribu kuwa mjinga, lakini sijui ni nini! Hicho ndicho kitu kile kile kilichowaangamiza Israeli katika safari yao, kilikuwa ni ule umati uliochanganyika.

¹⁵⁸ Na kama huo haukuwa ndio mfano wenyewe wa siku hizi, sijui ni nini! Umati uliochanganyikana, waaminio waliochanganyikana na wasioamini, “Kuwapeleka kanisani, maadamu watakuja na kubatizwa, hilo tu ndilo linalohitajika.” Ndugu, unapaswa kuwa umekufa kabla ya kuzikwa, umati uliochanganyikana.

¹⁵⁹ Ndipo Petro akasisimkwa sana, naye akasema, upesi sana, mara alipoona mambo ya kimbinguni, akasema, “Na tujenge hapa vibanda vitatu.”

¹⁶⁰ Upesi sana, jambo lile lile alilofanya Luther, jambo lile lile alilofanya Wesley, na jambo lile lile ndugu zetu wa Kipentekoste, sisi sote tulilofanya. “Loo, tutafanya awe Mpentekoste *huyu*, na

Mpentekoste *huyu*, na Mpentekoste *huyu*. Tutajiundia dhehebu letu.”

“Vema, hawa wanaamini Yeye anakuja juu ya farasi mweupe.”

“Vema, hatuamini, tunaamini Yeye anakuja juu ya wingu jeupe.”

“Vema, waacheni waende, hao si wa kwetu.” Loo, haya basi. Mambo ya kimbinguni yamefanywa.

¹⁶¹ Na halafu huyu hapa Bwana anakuja anatoa karama na kuwatuma watu fulani si muda mrefu uliopita, Ndugu yetu mpendwa Tommy Osborn, na Ndugu Roberts, na baadhi yao, ndipo walipotoka, na mambo ya kimbinguni yakaanza, kufanyika, ati nini? Wasingeweza tu kukaa katika madhehebu yao na kusonga mbele, muda si muda mwajua, iliwabidi kwenda kujitengenezea mvua ya vuli, na mvua ya masika, na mvua ya ndani, mvua ya nje, loo, jamani, jamani, mvua, mvua, mvua, mvua nyingi.

¹⁶² Ni kitu gani? Ya kimbinguni yamefanyika, ndipo umati uliochanganyikana unaanza. Hiyo ni kweli. Inawasisimua wa— watu; umati uliochanganyikana unaambatana nao.

¹⁶³ Sasa sikilizeni, wakati Petro alipokuwa akinena bado, alikuwa angali akinena hapo aliposema, “Na tujenge vibanda vitatu, kimoja cha Musa, na kimoja cha Eliya, na kimoja cha Yesu.”

¹⁶⁴ Na kabla hata hajamaliza kuzungumza, angalieni yale Maandiko yasemayo: “Alipokuwa akinena, Sauti ikanena kutoka Mbinguni, ikasema, ‘Sahau hilo.’” Vinginevyo, “‘Huyu ni Mwanangu mpendwa, msikieni Yeye.’”

¹⁶⁵ Msimsikie Musa, ninafurahia jambo hilo, nina furaha sana. Musa aliwakilisha torati, torati isingeweza kumwokoza mtu yeyote. Sheria ilikuwa ni polisi, sheria ilikuhukumu na kukufunga gerezeni, isingeweza kukutoa, neema inakutoa. Bali sheria inakufunga gerezeni, ilikuhukumu, neema inakutoa.

¹⁶⁶ Ndipo akasema, “Nitajenga maskani nyingine. Tutajenga moja kwa ajili ya wale wote wanaotaka kushika torati, na kuwaacha waende *huku*. Nao watakuwa na dhehebu hapa, washika sheria. Kisha tutakuwa na wale wanaowaamini manabii.”

¹⁶⁷ Sasa, Eliya aliwakilisha nini? Aliwakilisha haki ya Mungu. Alikuwa ni nabii mwenye nguvu, alipanda juu ya mlima, Bwana akamtuma huko juu. Mtu fulani akaanza kuingilia mambo ya Bwana, akimwambia aende wapi na afanye nini, ndipo Eliya akasimama, na kusema, “Kama mimi ni mtu wa Mungu, Moto na ushuke kutoka Mbinguni, uwateketeze.” Ndipo Moto ukashuka na kuwateketeza hamsini.

¹⁶⁸ Vema, wakarudi na kumwambia mfalme, akasema, “Loo, hilo, jambo ni kwamba, huenda—huenda—huenda kulikuwa na dhoruba ya joto, mwajua, ama *kitu kama hicho*, walipigwa na radi. Nitatuma wengine hamsini.”

¹⁶⁹ Kwa hiyo akatuma wengine hamsini, naye Eliya akasimama na kusema, “Kama mimi ni mtu wa Mungu, na ushuke Moto kutoka Mbinguni, uwateketeze.” Kisha wengine hamsini wakaenda. Hakukuwa na dhoruba ya joto wakati huo, mnaona. Mnaona, kamwe hawakuelewa. Lakini ilikuwa ni haki ya Mungu.

¹⁷⁰ Sitaki haki Yake, sitaki sheria Yake, nataka rehema Yake. Rehema ndiyo ninayoomba. Ee Bwana, usinihukumu kwa sheria yoyote, ni—nitahukumika, siwezi kustahimili, usi—usinipe haki, ni—ninapaswa kuwa... Ninapaswa kwenda jehanamu, kwa sababu mimi ni mwenye dhambi, lakini, Bwana, nipe rehema Yako, upendo Wako, neema Yako.

¹⁷¹ Mungu akasema, “Huyu ni Mwanangu mpendwa, msikieni Yeye, si Musa, si haki, si torati, bali msikieni Yeye, Yeye ana rehema kwa ajili yenu, Yeye ana karama kwa ajili yenu.”

¹⁷² “Alipaa Juu, na kuwapa wanadamu vipawa.” Naye Mungu amefanya vile vile hasa alivyofanya na Mwanawe wakati alipomkubali pale.

¹⁷³ Sasa, na vinginevyo, “Msinisikie tena, Mimi ni Mungu, bali nimempa Mwanangu mamlaka. Hakuna mtu awezaye kuja kwa Baba, ila kwa njia ya Mwana. Msikieni Yeye.”

¹⁷⁴ Loo, jamani, jinsi Mungu anavyotaka kulichukua Kanisa Lake leo na kulipa mamlaka! Amelizaa, sasa anataka kulipa mamlaka, bali kamwe hatutasimama kimya. Kama yakiinuka miongoni mwa Methodisti, Baptisti haitakuwa na uhusiano wowote nayo. Yakiinuka miongoni mwa kanisa moja, hilo lingine halitakuwa na uhusiano wowote nayo; ni mzunguko na mzunguko. Kwa nini? Ni umati uliochanganyikana, ungali ni kitu kile kile.

¹⁷⁵ Tunachohitaji siku hizi ni kukusanyika pamoja, na mkutano wa maombi, na kukaa pale mpaka Mungu atakapotuma kufanywa wana wenye mamlaka kwa Roho Mtakatifu, amshushe Roho Mtakatifu, na kuwaweka Kanisani mitume, manabii, waalimu, wainjilisti, wachungaji. Hilo ndilo tunalohitaji, hilo ndilo Kanisa linahitaji, Halitapatana, litadumu na Neno, Kanisa ambalo halitabembana na ulimwengu, Kanisa ambalo halitakuwa na uhusiano wowote na dhambi, ambalo litaipa dhambi kisogo, ambalo litatembea katika utakatifu na uzuri wa Mungu, wakimwishia Mungu. Niishi nife, inaleta tofauti gani, mradi tu niko upande wa Mungu, inaleta tofauti gani?

¹⁷⁶ Mungu anajaribu kuingiza jambo hilo kanisani, Yeye anajaribu kulifanya. Yeye hufanya hivyo mara kwa mara, kuwaonyesha tu watu ya kwamba Yeye analifanya. Basi ni kwa

nini, wakati Mungu anapozitikisa karama hizo mbele ya kanisa, halafu kanisa, kama nilivyosema hivi majuzi usiku, kama vile yule mtoto mchanga katika ninii, pamoja na yule mwanamke kwenye duka la mali rahisi hata linaonekana kutokulijali?

¹⁷⁷ Ijumaa, Jumamosi, Jumapili, Jumatatu, Jumanne, siku tano usiku, eneo hili kubwa mno hapa, na viti mia mbili vitupu katika jumba la mikutano la watu elfu moja mia mbili. “Kuona njaa na kiu ya haki.” Mnaona ninalomaanisha? Siwakemei, bali ninawaletea tu ukweli. Jambo ndilo hilo.

¹⁷⁸ Mnajua kuna nini? Ni kwa sababu kwamba watu watakuja kanisani, watu siku hizi wanataka burudani. Wamekuwa, Wamarekani wameburudishwa sana, hata hiyo ndiyo inayowabidi kuwa nayo. Hiyo—hiyo—hiyo inalisha roho iliyo ndani yao, ni roho iliyoburudishwa, inakubidi kuwaburudisha. Mungu hawaburudishi watu, Yeye huwakemea watu. Hukumu huanza katika nyumba ya Mungu. Na inapofikia wakati ambapo kanisa halina budi kuwa na milo ya supu, na dansi, na michezo ya karata, na kila namna ya upuuzi wa mauzo ya upekuzi kumlipa mhubiri, Mungu alirehemu kanisa hilo! Kweli. Hmm!

¹⁷⁹ Tunahitaji Roho Mtakatifu katika nguvu na kufanywa wana wenye mamlaka, ili huduma yetu inene. Amina. Lakini watu, wanapoenda kuona kitu fulani, wanaenda kuona hu—huduma fulani, “Hapa ndugu huyu ana huduma fulani.”

¹⁸⁰ Vema, wanaenda kule, wanasema, “Loo, naam, hilo—hilo ni zuri sana. Uh-huh. Ni sawa. Vema, sawa, tunaelekea wapi kesho?”

¹⁸¹ Kitu kingine. Mnaona? Hata haiwavutii hata kidogo. Wameona tu wema wa Mungu mwingi sana, mpaka wanatoka tu bila mpangilio.

¹⁸² Inanikumbusha juu ya hadithi ya kale ya Kiingereza, ilisema wakati mmoja kulikuwa na mtu aliyekuwa amesoma juu ya bahari, jinsi ilivyokuwa nzuri, jinsi yale mawimbi makubwa ya ajabu yenye chumvi nyingi, yangeruka, nao shakwe wangeruka juu, na ni jambo zuri jinsi gani, hakuwa amewahi kuona bahari.

¹⁸³ Na kwa hiyo yeye, siku moja a—alipata pesa za kutosha hata alikuwa anaenda baharini. Akashuka kupitia barani, mpaka akafika ninii, karibu na ufuo wa bahari, ndipo akakutana na mzee baharia, na huyo ni baharia, akitoka baharini, naye akasema, “Unaenda wapi, mtu wangu mwema?”

¹⁸⁴ Akasema, “Loo, nimesoma habari za bahari, ninaelekea baharini. Ninaenda kuona kwa macho yangu mwenyewe, mawimbi yake ya kuvutia, mazuri sana yanapopasuka, na mawimbi makubwa meupe ya maji ya chumvi. Ninaenda kusikia harufu ya hewa ya chumvi na kuyajaza mapafu yangu, na mimi, ninaenda kusikia mlio wa shakwe wa baharini,” na kadhalika. Loo, jinsi alivyofurahi sana kujua ya kwamba alikuwa anaenda kuona hiyo bahari kubwa.

Kwa hiyo, yule mzee baharia akamwanguka, na kusema, “Vema, nilizaliwa juu yake miaka hamsini iliyopita, sioni chochote cha kuvutia sana juu yake.”

¹⁸⁵ Mnaona, alikuwa ameiona sana, mpaka ikawa ni ya kawaida sana kwake, haikuwa ya kupendeza tena, ilikuwa ni bure. Alisimama tu pale, na kurukaruka juu ya mawimbi, wala hakuijali hiyo.

¹⁸⁶ Sasa, hivyo ndivyo kanisa limefikia kuhusu Mungu. Tunamwona Roho wa Mungu akishuka katika uamsho, na kuwatikisa watu, na wanasimama kutoka kwenye viti vya magurudumu, na—na viwete wanatembea, na vipofu wanaona, na Roho wa Mungu anashuka mkutanoni, anatambua mawazo yenyewe moyoni mwao, na mambo makuu ya kinabii yatatokea ambayo ni makamilifu kila wakati, vivyo hivyo hasa, nalo kanisa linasema, “Vema, hilo ni sawa,” lundo kubwa la chingamu, wameketi pale, mwajua, “nadhani hilo ni sawa. Lakini tutamwona Lucy kesho usiku, nasi hatutaninii...” Mnaona?

¹⁸⁷ “Mchungaji akitaka kutuhukumu, acha atuhukumu. Tutaenda kwenye dhehebu hili lingine, kama anataka kutuhukumu. Tutaenda kule na kujiunga na... Wakitufukuza kutoka Church of God, tutaenda kwenye Assemblies; wakitufukuza kutoka kwa Assemblies, tutaenda kwenye Umoja; wakitufukuza kwenye Umoja, tutaenda kwenye Uwili; nasi... wakitufukuza kutoka kwenye Uwili, tutaenda kwenye Utatu. Nasi tuna nafasi tele. Mnaona?”

¹⁸⁸ Naam, unayo nafasi, lakini, ndugu, kuna nafasi tu kwa ajili ya Kristo ndani yako, kama unataka kumjia Yeye. Loo, Mungu alirehemu kanisa la siku hizi. Nitakoma baada ya usiku wa leo, maana sitaki kuwakasirisha, lakini ili—ilinibidi tu kutumia siku hizi usiku kushindilia hili ndani yenu, kuwajulisha ya kwamba kanisa liko katika hali mbaya sana. Bila shaka ndivyo lilivyo. Bidii yetu, sisi ni wavivu tu, mwajua, wazembe tu. Mungu hataki tuwe hivyo. Anatutaka sisi... Ninawazia hili:

Usiniambie, kwa wingi wa maombolezo,
Maisha ni ndoto tupu tu!
Nafsi inayolala imekufa,
Na mambo sivyo yanavyoonekana.
Maisha ni halisi! Na maisha ni bidii!
Na kaburi sio lengo lake;
Kwa kuwa u mavumbi wewe, mavumbini
utarudi,
Haikusemwa juu ya nafsi.

Ninapenda ubeti huu wa hiyo *Zaburi Ya Maisha*:

Maisha ya watu mashuhuri yote
yanatukumbusha (Paulo, Petro, Yakobo,
Yohana.)

Maisha ya watu mashuhuri yote
 yanatukumbusha
 Tunaweza kuyafanya maisha yetu adhimu,
 Tunapoachanana tunaacha nyuma yetu
 Kumbukumbu za kudumu;

Kumbukumbu ambazo labda mwingine,
 Huku akisafiri kwenye bahari kuu ya maisha,
 Kwa ndugu mpweke aliyeharibikiwa na meli,
 Katika kuziona nyayo zenu, atajipa moyo tena.

189 Ni walevi wangapi wangeona nyayo za mlevi aliyeongoka na anaishi maisha matakatifu na ya kitaua? Ni wanawake wangapi wangeshikilia wanapomwona mwanamke mwaminifu akisimama, amevaa kama mama wa heshima, na kutenda kama mama wa heshima, na kwenda kanisani, huku moyo wake wote umetolewa kwa Mungu? Hapo ndipo unapotiwa muhuri, hapo ndipo unapotiwa alama, kila mtu anakujua. “Ninyi ni chumvi ya dunia, lakini ikiwa chumvi imepoteza ladha yake, haifai kitu, hutupwa nje, chini, kukanyagwa chini ya miguu ya watu.”

190 “Mungu, jalia kanisa la Kipentekoste liishi,” ndilo ombi langu. Jalia atufikishe mahali fulani, laiti angelifanya papa hapa usiku wa leo, laiti angelichukua kundi hili moja kwa moja hapa ndani usiku wa leo na kutufanya wana wenye mamlaka, kutupatia mamlaka kama wana na binti Zake. Tumezaliwa wana na binti Zake, lakini hebu Yeye atupe mamlaka kama wana na binti. Huu ungetokea kuwa mkutano wenye nguvu jinsi gani!

191 Jinsi Mungu angeweka karama katika kanisa hili papa hapa usiku wa leo ambazo zingeninii, mbona, kufikia wakati huu kesho kutwa usiku, kuna kitu fulani... kila mtu aliye karibu na hapa angejua jambo fulani lilikuwa likiendelea kwenye jengo hili la shule hapa, hakika angejua. Wangejua hilo, kwa sababu kwamba Roho wa Mungu alikuwa akiishi miongoni mwa watu.

192 Loo, jinsi ninavyotaka kufanya hivyo! Hivi hamtaki hilo, kila mmoja wenu? Msinikasirikie kwa kuwa tu fidhuli sana nalo. Lakini kama nilivyosema daima, ndugu yangu hapa anasema, seremala, usipopigilia msumari kwa nguvu, hautashikilia, utalegea mara moja. Kwa hiyo, natumaini hili halitalegea, natumaini litakaa papo hapo, papo hapo, na mlishikilie moja kwa moja kwa mikono miwili.

193 Inanikumbusha, miaka mingi iliyopita nilikuwa nikienda huko Colorado katika misimu ya mwanzoni kuwinda. Nami ninapenda kuwinda paa na kulungu, na ningechukua likizo yangu. Siku moja, niliona mandhari huko juu ambayo sijawahi kusahau. Nilikuwa, imekuwa miaka kadhaa iliyopita, nilikuwa huko juu ukingoni nyuma ya Continental Divide, na kuna kile wanachokiita Mto Troublesome. Nilikuwa kwenye ranchi mle ndani katika, kwenye...

¹⁹⁴ Kijito cha mashariki na cha magharibi hufanyiza Mto Troublesome, nalo Shirika la Hereford hulisha humo bondeni. Kama unaweza kuchangia tani moja ya nyasi kavu, unaweza kuweka ng'ombe humo malishoni. Na kila ranchi imepimiwa tani *kadhaa* za nyasi kavu, nanyi, nadhani hivyo ndivyo mnavyofanya hapa Oregon, unamweka ng'ombe wako malishoni.

¹⁹⁵ Nilikuwa nikienda huko juu wakati wa kukusanywa kwa mifugo, wakati alipokuwa akiwachukua kuwapeleka ng'ombe wa msimu wa kuchipuka kuwakusanya. Basi kulikuwako na uzio wa kutenganisha mali ya watu binafsi na ya serikali, nami ningeleti pale, mguu wangu kwenye ncha ya tandiko, na kumwangukia yule mlinzi alipokuwa amesimama pale, akiwaangalia hao mifugo wakipita.

¹⁹⁶ Sasa, yetu ilikuwa ni Tripod, na Bw. Grimes kule juu alikuwa ni Diamond Bar, na, loo, walikuwa na wafugaji ishirini ama thelathini mbalimbali waliokuwa wamepitisha mifugo yao. Sasa, niliona mfugaji huyo kamwe hakujali sana ni chapa gani iliyokuwa kwenye ng'ombe. Mnajua kile alichangalia? Aliangalia kibandiko cha damu sikioni. Mnaona? Hereford halisi, la sivyo asingeweza kwenda kwenye malisho hayo.

¹⁹⁷ Nami nafikiri hivyo ndivyo Mungu atakavyofanya kwenye Siku ya Hukumu, Yeye hatajali kama wewe ni mfuasi wa—wa Assemblies, ama wa Church of God, ama wewe ni wa nani, Yeye atachunguza hicho kibandiko cha Damu, ndugu. Na kama hicho kipo pale, utaingia; la sivyo, sijali umevaa chapa gani, utakataliwa, hivyo tu.

¹⁹⁸ Kwa hiyo, siku moja huko juu, huko juu kabisa mlimani, ni...yule mzee mfugaji tulikuwa marafiki wazuri sana, mwindaji hodari. Naye alikuwa amechukua farasi wa mizigo akaenda zake kwenye mlima wa magharibi, nami nilikuwa huko chini kwenye milima ya mashariki, ile tunayoita Vilele vya Corral. Wala theluji haikuwa imeanguka bado, na, ama ya kutosha kudumu, ilikuwa ni mapema, nazo dhoruba za theluji hazikuwa zimekuja, kwa hiyo wanyama walikuwa huko juu.

¹⁹⁹ Nami nilikuwa nimemfunga farasi wangu, na nikaenda safari ya siku moja karibu na mpaka wa msitu. Na kwa hiyo, zikatokea, moja ya hizo dhoruba za Oktoba, za msimu wa kupukutika, na halafu labda itanyesha kwa nguvu sana iwezavyo, halafu mvua ya theluji, kisha theluji, halafu jua lichomoze, halafu mvua tena, mnajua jinsi ilivyo katika majira ya kupukutika.

²⁰⁰ Ndipo dhoruba ikaja, nami nilikuwa huko juu sana, mpakani mwa misitu, kukavu sana nisingeweza kuona miburuzo, kwa hiyo, nilikuwa, nikaingia nyuma ya mti na kidogo nikajipinda nyuma ya huo mti namna *hii*, huo ni msemu mbaya sana, lakini nilikuwa nimesimama nyuma ya mti kuweka bunduki yangu

chini. Dhoruba ikapita, ndipo baada ya dhoruba kupita, ikawa baridi wakati dhoruba ilipokuwa ikiendelea, nayo ikanyesha kwa nguvu sana, ndipo baada ya dhoruba kuja nilikuwa nimesimama pale nikiwazia juu ya Mungu, nikawaza, “Ee Mungu, jinsi Wewe ulivyo wa ajabu!” Daima ninamwona Mungu katika maumbile, hapo ndipo unapomwona. Nikawaza, “Wewe ni wa ajabu sana, Bwana. Loo, laiti ungalinishukia hapa, na kunijalia niende Nyumbani kutoka hapa.” Nikawaza, “Hebu. . .”

²⁰¹ Nikifa, wayakariri maombi ya Wahindi juu yangu nitakapokufa, “Bwana Mungu, Baba mkuu Mwenye Roho, jalia atembe kwenye mburuzo wa wanyama, na kukutana na wapendwa wake Ng’ambo ile.”

Nikawazia, “Naam, Bwana, jalia niende kwenye Nchi kama hii nitakapouacha ulimwengu huu.”

²⁰² Nami nilikuwa tu nimesimama pale, dhoruba ikaachilia, nami nilikuwa nikiichunguza kwa bidii sana, kwa hiyo nikasimama, nikaangalia kote, ndipo ikawa nilitambua kwamba. . . niliangalia ng’ambo upande *ule* kuelekea magharibi, kuelekea Oregon hivi, na mwanya milimani, karibu mwisho wa alasiri. Jua likipitia pale kama jicho kubwa mno, kama Mungu, “Jicho lake liko kwenye shorewanda.” Nikawazia, “Ee Mungu, Wewe huyo hapo kwenye machweo ya jua.”

²⁰³ Ndipo nikaangalia, na ambapo m—mvua ilikuwa imeganda kwenye mti usiokauka, hapo ukatokea upinde wa mvua, ukivuka lile bonde. Huko juu kabisa mlimani maskini mbwa mwitu wa kijivu akalia, mwenziwe akamwitikia huko chini kabisa. Maskini kulungu dume akaanza kulia, alipotea wakati wa dhoruba namna hiyo. Nena kuhusu kilindi kuita kilindi! Loo, jamani!

Nikawaza, “Kwa nini inilazimu kuondoka mahali hapa? Hapa ni nyumbani kwangu, laiti ningaliweza kukaa hapa milele.”

Nikajisikia kama Petro alivyojisikia, “Na tujenge vibanda vitatu, na tukae tu hapa. Hapa ndipo mahali pa kukaa.”

²⁰⁴ Nilimsikia Mungu katika mwito huo wa mbwa mwitu, akimwita mwenziwe, nikawaza, “Naam, Mungu, huyo ni Wewe ukiniita.” Nilimsikia yule kulungu vivyo hivyo, nikaona upinde wa mvua ukipita, nami nikawazia, “Upinde wa mvua maana yake ni agano. Wewe ni Alfa na Omega, Mwanzo na Mwisho, miisho yote miwili ya upinde wa mvua, Yeye Aliyekuwako na Ambaye anakuja, Shina na Mzao wa Daudi, ile Nyota ya Asubuhi, Yungiyungi la Bondeni, Ua la Uwandani,” loo, jamani, yote aliyokuwa.

²⁰⁵ Ndipo nikawazia, “Katika upinde wa mvua, lile agano, kama wanavyomwona Yeye katika Ufunuo 1, pale alionekana kama upinde wa mvua, kama wa Kwanza na wa Mwisho, Benyamini

hadi...na kutoka kwa Reubeni hata Benyamini, wa Kwanza na wa Mwisho.”

206 Na, loo, ni, Maandiko yakimiminika tu, nikawaza, “Ee Mungu, Wewe ni mkuu sana! Wewe ni mkuu sana!” Nikaanza kukanyaga miguu yangu juu chini, kuzunguka, nikauzunguka mti huo, upesi tu nilivyoweza kwenda, upesi tu niendavyo, nikipaza sauti, “Haleluya! Haleluya! Haleluya! Haleluya!” Nikikimbia tu namna hiyo. Nikasimama, nami nikasema, “Ee Mungu, jinsi Wewe ulivyo mkuu! Haleluya! Haleluya! Haleluya!”

207 Loo, nilikuwa kama Jeshi zima la Wokovu kule juu, nilikuwa na wakati mzuri. Sikuwa makini na yale mtu mwingine yeyote, mbona, nilikuwa maili thelathini na tano, arobaini kutoka kwenye ustaarabu, nilikuwa nikipiga makelele kwa Bwana. Hivi hamwamini Wabaptisti hupiga makelele? Mlipaswa kunisikia.

208 Kwa hiyo, nilizunguka mahali pale tena na tena, upesi tu nilivyoweza kwenda, nikipiga makelele ya sifa za Mungu. Nikawaza, “Loo, ni ajabu jinsi gani! Jinsi ningependa kukaa hapa, Bwana! Loo, kama sikuwahi kuwa na kampeni nyingine, nikae tu papa hapa pamoja Nawe, mpaka utakapokuja na kunichukua! Ni ajabu jinsi gani!” Lakini, kama tu vile Petro na hao wengine kwenye siku ile, huko chini ya mlima kulikuwako na mvulana mgonjwa wa kuponywa, kwa hiyo ninajua ilinibidi kurudi katika siku chache.

209 Nami nilikuwa nimesimama pale, ndipo mara moja, maskini kuchakulo wa misonobari, sijui kama mnao hapa ama hamna, loo, yeye ni polisi wa koti la samawati wa mwituni, kitu chenye kelele sana nilichopata kusikia, akaruka juu, kulikuwako na maskini uwazi pale, naye akaruka juu ya kisiki, akaanza kwenda, “*Kwee, kwee, kwee! Kwee, kwee, kwee! Kwee, kwee, kwee!*”

210 Ndipo nikawazia, “Unasisimkwa na nini hivi, ewe jamaa mdogo? Mbona, wewe si mkubwa vya kutosha kufanya lolote. Kwa hiyo unapiga kelele za nini?” Nikasema, “Loo, una—unapayukia nini? Au nilikutisha? Kama hukulipenda hilo, angalia hili kidogo, hebu nikuonyeshe jinsi kweli ninavyoweza kuendelea.” Ndipo nikazunguka na kuzunguka ule mti tena. Nikawaza, “Unapendaje hilo?” Nikasema, “Loo, jamani, Muumba wetu ni wa ajabu, unapaswa kumsifu.”

211 Lakini niliona hakuwa akiniangalia, angeinamisha maskini kichwa chake upande, na jicho hilo limetokeza shavuni mwake, mwajua, akiangalia chini namna *hiyo*. Na baada ya kitambo kidogo, akitambaa kutoka hapo, upepo ulikuwa umemshusha chini tai mkubwa wa hudhurungi, loo, hao ni ndege wa kupendeza, nampenda tai, naye akaruka juu ya huo. Nami nikawaza, “Loo, kumbe hivyo ndivyo ilivyokuwa. Uh-huh. Hilo ndilo ulilokuwa ukiendelea nalo, ulimwogopa huyo tai.”

²¹² Tai huyo mkubwa akaruka juu pale, na loo, ni jamaa mkubwa mno, mkubwa jinsi gani, hayo macho makubwa ya kijivu, yakiopesa pande zote. Nikawazia, “Bwana, kwa nini umeondoa usikivu wangu kutoka kwenye upinde wa mvua, na kutoka kwa mbwa mwitu, na yote haya, ili tu...kwa huyu hapa? Kuna nini cha kitaua kuhusu tai huyo?” Ndipo nikawazia, “Sioni kitu chochote cha kitaua kuhusu maskini kuchakulo huyo mdogo; sioni chochote cha kiungu kuhusu yule tai. Ni kitu gani cha kitaua sana kwake?”

²¹³ Ndipo nikaanza kuona, nikawazia...Nikamwangalia, nikasema, “Je, ulijua ningeweza kukupiga risasi?” Nikasema, “Hii *hapa* bunduki yangu imewekwa, ningeweza kukupiga risasi.” Alijua vizuri zaidi ya hayo. Hilo halikumsumbua hata kidogo. Nikawaza, “Hivi huniogopi? Uliogopa kwa sababu nilikuwa nikipaza sauti namna hiyo? Huyo alikuwa ni Muumba wetu, ninamsifu tu, unapaswa, pia.” Nami ninaninii tu...

²¹⁴ Kama mtu angalikuja mwituni, wangepikiri walikuwa na mwendawazimu huko nje. Lakini sikujali, nilikuwa na wakati mzuri, nilikuwa nikimwabudu Bwana. Hiyo ndiyo shida ya...tuna woga kupita kiasi na woga mwingi kupita kiasi. Tunamhitaji Mungu, tunahitaji kutambua ya kwamba hakuna mtu hapa ila mimi na Mungu, hivyo tu. Hivyo tu. Hiyo ni kweli.

Tunaanza kushangaa, “Jirani atasema nini kunihusu mimi?”

Ishi vema, naye jirani atajua kinachotokea, kwa vyovyote vile, wanapoambatana nawe.

²¹⁵ Kwa hiyo basi, nikamsikiliza maskini kuchakulo huyo mdogo, mwajua, nami nikamwangalia pale; yule tai, nikawaza, “Ni kitu gani kinachokufanya u—ujiamini sana?”

²¹⁶ Ndipo nikaanza kumwona, angeyafanya hayo mabawa makubwa, mwajua, hayo manyoya, kuyatimua namna *hiyo*, mwajua, kwa namna fulani akiyanyosha. Nikawaza, “Kumbe, uh-huh. Una matumaini katika mabawa hayo. Unajua kabla sijaweza kuigusa bunduki hiyo, na kuiweka begani mwangu, ungekuwa kwenye ile miti kule, nisikuone tena.” Unaona?

²¹⁷ Nikawazia, “Kama unaweza kuwa na matumaini kiasi hicho katika hayo mabawa, kwa sababu Mungu amekupa mabawa ukwepe hatari, Kanisa la Mungu linapaswa kuwa na ya kiasi gani katika nguvu za Mungu ambayo yanaweza kuwafanya waepuke maradhi, na magonjwa, na shida, na mauti, na kuzimu, na kuruka kwenda kwa Mungu siku moja mikononi mwa Bwana Yesu!” Ninii tu, nikawaza, “Yeye—yeye anaendelea kuhisi, mradi tu anaweza kuyahisi hayo mabawa yakiwa tayari kwa kuruka, alikuwa sawa, alijua mahali alipokuwa amesimama.”

²¹⁸ Na hata hivyo Roho Mtakatifu anaweza kushuka juu ya kanisa, nao watajirudisha nyuma, “Loo, sijui, ukiniombea tena, labda yote yatakuwa ni sawa.” Unaona? Hiyo ni ninii tu, loo, jamani, ni mbaya sana, naam, bwana.

219 Nilimwangalia pale kitambo kidogo, nitawaambia kilichompata jamaa huyu, nikamwangalia kwa muda kidogo, nikaangalia pale, nami nikawazia, “Loo, ninavutiwa nawe. Ninakuona Wewe katika huyo tai, Mungu.”

220 Na kwa hiyo, baada ya kitambo kidogo, hakuniogopa, naye aliona ya kwamba... Ni—ni—nilimpenda. Ninavutiwa na chochote kilicho na ninii—kilicho na uti wa mgongo kwake. Ninachukia kumwona mtu akiya kanisani na kuninii tu, loo, sifa zote na kadhalika, akirudi na kuona aibu kushuhudia mtaani, ukiona aibu kuombea chakula unachokula kwenye mkahawa, loo, jamani, kwa woga. Mungu hawezi kumtumia mwoga, anataka wanaume. Anataka kuutoa huo mfupa wa shingo ya kuku, na kuweka uti wa mgongo hapo ndani.

221 Kama vile mzee Buddy Robinson alivyosema, “Bwana, nipe uti wa mgongo ukubwa wa gogo la msumeno, weka maarifa mengi mwishoni mwa ukuta wa nafsi yangu, na kunisaidia kupigana na ibilisi mradi tu nina jino, kisha nimwume kwa ufizi mpaka nife.” Kwa hiyo hiyo ndiyo aina ya ushuhuda ambao sote tunapaswa kuwa nao. Mnamkumbuka Buddy Robinson, wengi wenu, yule ndugu wa Kinazarayo?

222 Sasa, nilimwangalia maskini yule tai ndipo nikawazia, “Vema, unajua, wewe kweli ni ndege mwenye neema, na—nawapenda sana. Nilihubiri juu yenu mara nyingi.” Kisha nikasema, “Hakika na—nakupenda sana.”

223 Akachoka kumsikiliza maskini kuchakulo huyo wa misonobari akifanya, “*Kwee, kwee, kwee! Kwee, kwee, kwee!*” kana kwamba alikuwa akitaka kumrarua. Mbona, asingeweza kufanya lolote, yeye ni mdogo sana. Akatosheka nayo, kwa hiyo akafanya tu mruko mmoja mkubwa, akapiga mabawa yake karibu mara mbili, ndipo basi nikalia.

224 Nilisimama pale huku machozi yakitiririka mashavuni mwangu nilipomwangalia tai huyo. Jinsi hapana shaka Mungu alimweka pale kwa kusudi fulani! Kamwe hakupigapiga mabawa yake, aliruka tu juu ya huo msitu, yapata mara mbili, na ndipo akajua tu jinsi ya kuweka mabawa yake katika upepo huo, na kila wakati upepo mkali ungevuma, angepanda juu kidogo, juu kidogo, na juu kidogo, mpaka akafanyika doa dogo tu.

225 Akamwacha huyo kuchakulo mdogo wa misonobari wa duniani, ameketi pale akifanya, “*Kwee, kwee, kwee!* Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama Roho Mtakatifu. Loo, hakuna... Huku kunena kwa lugha si sawa kabisa. Hakuna kitu kama Pentekoste, hiyo ilikuwa ni huko nyuma muda mrefu uliopita.” Alijua tu jinsi ya kuweka mabawa yake katika nguvu za huo upepo.

226 Ni jinsi gani kanisa linapaswa kujua jinsi ya kuweka imani yenu katika nguvu za Mungu! Sio kuruka kutoka kanisa moja hadi lingine, bali kuabiri juu ya utukufu wa Mungu, mpaka

umepita kusikia kwa upuuzi huu wa, “Siku za miujiza zimepita, hakuna kitu kama Roho Mtakatifu,” upuuzi.

²²⁷ Unawazia nini kuhusu hilo, mama? Unaamini hilo kuwa ni kweli? Unaamini hilo, pia, dada? Kama unaamini, unaweza kuruka kutoka kwenye hayo machela usiku wa leo ukitaka.

²²⁸ Ninii tu, si kwenda kwenye mkutano *huyu*, kwenda kwa *ule*, kumfanya *huyu* akuombe, ama *yule* akuombe, mhubiri fulani *huyu*, *yule* mwinjilisti fulani. Weka tu mabawa yako, weka imani yako, “Sitatikisika.” Haleluya! Na kila wakati Roho Mtakatifu anapoingia, panda juu Yake, kwenda juu zaidi, na juu zaidi, na juu zaidi, na juu zaidi. Jambo ndilo hilo.

²²⁹ Unaamini hilo kwa moyo wako wote? Kama unaamini, ndugu, jua tu jinsi ya kuweka mabawa yako. Mungu aliahidi, Mungu hawezi kusema uongo, Mungu ni kweli yote. Kama ningeweza kukuponya, ningefanya hivyo. Siwezi kumponya mtu yeyote, Siamini kuna mtu mwingine yeyote anayeweza kumponya mtu yeyote. Lakini ni wewe, wewe mwenyewe, wewe, mwenyewe, unayemwamini Mungu. Roho Mtakatifu amekuwa tu daima akishuka katika jengo hili usiku wa leo. Unaamini hilo? Hakika. Hata akilikemea na kulirudi Kanisa Lake na kulisafisha. Hivyo ndivyo Mungu anavyotaka kufanya.

²³⁰ Maskini wapiga dhahabu, hivi mnajua jinsi walivyokuwa wakijua ilikuwa ni dhahabu halisi, nzuri? Wangechukua dhahabu hiyo, na kuitwanga, na kuitwanga, na kuigeuza, na kuitwanga, mpaka wakatwanga na kutoa takataka zote kutoka kwake. Mnajua jinsi wanavyojua wakati wametoa takataka kwake? Walipoona uakisi wao wenyewe ndani yake, ndipo wakajua ya kwamba kimbwi yote, na kadhalika, ilikuwa imetoka. Mawe yote na nyenzo zilikuwa zimetoka, ilikuwa dhahabu safi, wakati mpigaji angeweza kuona uakisi wake.

²³¹ Hivyo ndivyo Kristo anavyolitendea Kanisa Lake, Yeye analitwanga, na kuligeuza, na kulipiga, na kulipindua, na kulitwanga. Mhubiri anathubutuje kuwa dondoadume vya kutosha asilielezee Neno la Mungu, na kuwaambia wanaume na wanawake wakati wanaishi vibaya! Awaambie ni vibaya kuvaa nguo hizi chafu, ni vibaya kuvuta sigara, ni vibaya kukaa nyumbani usiende kanisani, ni makosa kwenda kucheza kamari, na mashindano ya mbio za farasi, na kufanya jinsi kanisa linavyofanya siku hizi, na kucheza bahati nasibu, na kadhalika. Mungu anizuie wakati inanibidi kufanya hivyo. La, bwana.

²³² Kitwange Kitu hicho mpaka, Yesu anakitwanga kwa Roho Mtakatifu mpaka aone uakisi Wake Mwenyewe ndani Yake. Ndipo unaweza kuona kazi za Kristo zikifanywa Kanisani, ndipo liko tayari kwa ajili ya Unyakuo, dhahabu safi. Mnaamini hilo, ninyi nyote?

²³³ Vema, ni wagonjwa wangapi walio hapa ndani? Inueni mikono yenu. Mlisema mlikuwa waaminio, sivyo? Vema,

nitawaomba mfanye jambo fulani. Ninyi—ninyi wachungaji wawili, nawatakeni mje kwenye kitanda *hiki* cha wagonjwa. Ninyi wachungaji wawili, nawatakeni mwende kwenye kitanda *hiki* cha wagonjwa. Niwaonyeshe si wanadamu. Amina.

²³⁴ Sasa, watu hawa ni watu wanaoamini, hawa wengine wanaamini pia, bali niliwachagua hao wawili. Wawili ni shahidi. Vema. Ni wangapi kati yenu wengine mnaoamini sasa? Vema.

²³⁵ Sasa, Neno la Mungu ni kweli? Hakika, ni kweli. Ni kweli. Sasa, kama... “Kuomba kwa imani kutamwoko mgonjwa yule.” Hiyo ni kweli? “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Hiyo ni kweli? Sasa, kama hilo si kweli, basi hujaokoka, Mungu yeye yule alilisema. Mnaona? Kwa hiyo hujaokoka, hakuna Mbingu, hakuna—hakuna mambo ya baadaye kama hiyo si kweli.

²³⁶ “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, wakiweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya,” sasa, kila mtu ambaye ni mwaminio. Haikusema, “Ishara hizi zitafuatana na wahudumu.” “Ishara hizi zitafuatana na *hao*,” hata iwe ni nani, “waaminio, wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.”

²³⁷ Unangojea maombi kwa ajili ya mtoto huyo mchanga, sivyo, dada? Huyu mtoto alikuwa ni mgonjwa, ama kitu fulani, ulitaka aombewe? Huyu mtoto mchanga? Ni mgonjwa sana? Wewe ni mhudumu, ndugu? Vema, nenda ukaweke mkono wako juu ya maskini mtoto huyo mchanga, mwenye nywele nyekundu pale chini. Ninaangalia pande zote nione kama ninaweza kumwona mtu mwingine anayetaka kuwekewa mikono.

²³⁸ Vema. Sasa, kwa kawaida tunachukua upambanuzi. Nasi tungeweza kuufanya sasa hivi, pia. Loo, hakika, bila shaka. Hilo ni—ni sawa tu kama—kama—kama sisi—kama tunaliadini, bali inakubidi kuliadini. “Kama unaweza kuamini, yote yanawezekana.”

²³⁹ Sasa, kumbukeni ya kwamba kama tukisali na kumwomba Mungu kwa uaminifu, kanisa hili, sasa, sisi ni kitu kimoja, tuko pamoja, tukimwomba Mungu kwa uaminifu, basi Mungu anawajibika kushughulikia yale tuliyo—tuliyoomba. Hiyo ni kweli? “Mkiomba lolote katika Jina Langu, nitalifanya.” Je, hiyo ni kweli? Ngojeni tu. Je, hiyo ni kweli? Hakika. Nitamtumainia nafsi yangu, nimefanya hivyo. Miaka thelathini na mmoja, niliishi kwa matarajio juu ya haya...katika Yohana Mtakatifu 5:24. Ukitaka kulisoma, wazia tu konzi moja na dazani mbili za mayai, unaona.

²⁴⁰ Yohana Mtakatifu 5:24:

...*Yeye alisikiaye neno langu na kumwamini yeye aliyenipeleka yuna uzima wa Milele, wala hataingia hukumuni; bali amepita kutoka mautini kuingia uzimani.*

²⁴¹ Ninaamini hilo. Mimi, kama mvulana mdogo, nilifanyika mhudumu, mvulana tu, nilihubiri tangu wakati huo, kuyatoa maisha yangu kwa ajili ya Injili. Laiti ningalikuwa na maisha elfu kumi ya kumtolea. Ni ajabu kweli, Ninayafurahia, kila sehemu yake. Sasa, unaweza... wewe... Kama *hilo* sivyo, basi mimi... Kama *hilo* sivyo, basi *hili* lingine sivyo lilivyo; kama *hili* sivyo lilivyo, basi *lile* sivyo lilivyo; kama *hili* ni *lile*, basi *lile* ni *hili*, mnaona. Kwa hiyo tuko—tuko—tuko tayari.

²⁴² Mko tayari kuomba? Vema, sasa, kila mtu hapa ndani, ninakutaka umwekee mikono mtu fulani aliye karibu nawe. Nanyi ndugu, ninataka kila mmoja mguuni, na mmoja kichwani mwa haya machala hapa, mwekeeni mikono maskini—maskini huyo mvulana mdogo hapo, juu ya watu hawa. Sasa hebu na tusimame.

²⁴³ Loo! Ninapenda sana wakati wa namna hii, kitu fulani tu, kila mtu ameshikilia pumzi, kitu kama, “Itakuwaje?” Angalieni kinachotukia. Kama ukigeuka tu... Achilia tu imani yako huru sasa, acha tu imani yako ishuke moja kwa moja, useme, “Dada *huyu* ataponywa. *Huyu* ataponywa. Mwanamume *huyo*, mwanamke *huyu*, *huyu*, na *huyu*, na *yule*, na *yule*, wote wataponywa. Wataponywa, huu utakuwa ndio mwisho wake. Kesho kutakuwa na tofauti kubwa sana katika watu hao, mbona, jamani itakuwa ni ajabu.” Hivi hamwamini hilo?

²⁴⁴ Sisi ni nini? Kanisa la Mungu. Tunajuaje sasa, ya kwamba Mungu hatamfanya kila mmoja wetu usiku wa leo mwana mwenye mamlaka, tunapofanya jambo hili? Tunatii amri Zake.

²⁴⁵ Sasa, kila mmoja wenu, kama tu kwamba ilikuwa ni nanii wako... Usijiombe mwenyewe sasa, wewe mwombe mtu ambaye ameweka ninii yako... mikono yao juu yako. Sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu, kila mmoja sasa, huku wamewekeana mikono. Ninawatakeni ninyi nyote kurudia ombi hili nyuma yangu:

²⁴⁶ Mwenyezi Mungu, Muumba wa Mbingu na nchi, Mwanzilishi wa Uzima wa Milele, Mpaji wa vipawa vyote vyema, Baba Yangu, nipe imani kwa ajili ya mtu niliyemwekea mikono yangu. Jalia niamini kwa moyo wangu wote ya kwamba mtu huyu ataponywa kwa nguvu Zako. Kama nimetenda dhambi, nikakosa kukuamini Wewe kwa njia yoyote, nisamehe. Nitakupa sifa zote na utukufu wote. Ninaahidi jambo hili, katika Jina la Yesu. Amina.

²⁴⁷ Sasa, endeleeni kuinamisha vichwa vyenu. Sasa, mnajua yale mmesema. Sasa, m—mlisema kwamba, sasa, hayo ndiyo ma—maombi ambayo Mungu huweka kupitia midomoni mwako kwa mtu huyo, basi kumbuka, huyo mtu mwingine alikuombea jambo lile lile. Sasa jifungie ndani pamoja na Mungu, hakuna mtu humu ndani ila wewe na Mungu sasa. Ninii tu—ninii tu, kwa imani, hisi nguvu hizo za Mungu zikishuka chini katika miili hiyo migonjwa. Roho Mtakatifu, uliyemhisi dakika chache

zilizopita, unamhisi sasa hivi? *Kusogea* huko, hiyo hisia ya *kutuliza* ikipitia ndani yako, ikiuchochea mwili wako, hizo ni nguvu Zake za uponyaji.

²⁴⁸ Ee Mungu, Wewe uko karibu. Yehova mkuu, Wewe ni Mungu wa milele, mtume Roho Wako Mtakatifu sasa, Bwana. Jalia kila mtu humu ndani ajazwe na nguvu Zako, hata zitasogea kutoka mkono hadi mkono, kutoka mahali hadi mahali, mpaka wote walio wagonjwa wapate kuponywa, ndipo watajua, ya kwamba uponyaji si wa mwanadamu, ni Mungu.

²⁴⁹ Wanaombeana wao kwa wao. “Kuomba kwa imani kutamwoko mgonjwa yule, Mungu atawainua; kama wamefanya dhambi yoyote, watasamehewa.” Tujalie, Bwana. Yasikie maambi yetu. Ninawaombea wote, ninawaombea ndugu zangu wahudumu, na kila mmoja ambaye amemwekea mikono mtu fulani, kwamba Roho Mtakatifu atakuwa halisi sana kwao, hata wataweza kuhisi nguvu za Mungu, naye atawapa ujasiri sana, mpaka hii itakuwa ndiyo saa ya kufanywa wana wenye mamlaka kwa kundi hili la watu, kwamba watafanywa wana wenye mamlaka wapate nguvu, katika maeneo ya Bwana Yesu Kristo, ili kwamba nguvu za Mungu zipate kupitia kila mmoja sasa, na kila mmoja wao aponywe.

²⁵⁰ Loo, uko karibu, Bwana, uko hapa, ninajua bila shaka yoyote ya kwamba uko hapa, na nguvu Zako sasa zinaingia, zikibariki. Kile ulichobariki kitabarikiwa, unachosema kitafanywa, kile mnachoweka mioyoni mwenu, hivyo ndivyo itakavyokuwa. Na iwe, Bwana.

²⁵¹ Tunamwapisha Shetani, Ewe ibilisi, ewe pepo mwovu, mshtaki, ambaye amewafunga watu hawa, wewe ambaye umefanya uovu huu, umeshindwa vita, Yesu Kristo alikufa, na naam, akafufuka tena katika siku ya tatu, na kukunyang'anya kila haki halali uliyo nayo. Wewe si kitu ila mdanganyifu, nasi tunakupa changamoto usiku wa leo, Shetani. Ewe pepo mchafu, waachilie watu hawa! Tunakuamuru, katika Jina la Yesu Kristo, ya kwamba kila shaka litafagiliwa mbali kutoka kwa watu hawa sasa hivi, naye Roho Mtakatifu ataingia miilini mwao na kumweka kila mmoja wao huru kutokana na maradhi, na kutokana na ugonjwa, na maumivu, na mateso, na kutoka kwa nguvu za uovu!

²⁵² Loo, Shetani, umeshindwa, katika Jina la Yesu, umeshindwa, umepotea. Wewe ni—wewe si kitu ila laghai, nasi tumekupa changamoto. Toka, tunasema, tunakuamuru, katika Jina la Yesu, uondoke kwenye kusanyiko hili!

²⁵³ Na wagonjwa wote na wanaoteseka waponywe kwa utukufu wa Mungu.

²⁵⁴ Haleluya! Haleluya! Haleluya!

Ninaweza, nitaamini, ninaamini;
Ninaweza, nitaamini, ninaamini

Kwamba Yesu ananiponya sasa.
 Tabibu Huyo mkuu sasa yuko karibu,
 Yesu mwenye huruma;
 Yeye hunena mioyo iliyohuzunika ipate
 kushangilia,
 Hakuna jina lingine ila la Yesu.

²⁵⁵ Kama usingeweza kusogeza kidole, kisogeze sasa. Kama usingeweza kusikia ila kwa sikio moja, weka kidole chako kwenye hilo lingine. Ama haidhuru wewe ni nini, kamwe hutafanya vizuri zaidi mpaka uifanyie mazoezi imani yako. Mpe Mungu nafasi kwako sasa, mpe Mungu nafasi ya kukufanyia jambo fulani. Maombi ya imani yameombwa, umewekewa mikono.

²⁵⁶ Na sasa, kwa amri ya Bwana Yesu, ninaamuru kwamba ibilisi awaache, na kila mmoja wenu aponywe! Amina.

²⁵⁷ Mnaliamini? Kila mtu anayeamini hilo, simama kwa miguu yako, na ukubali uponyaji wako sasa, katika Jina la Bwana Yesu. Amina.

²⁵⁸ Jambo ndilo hilo. Haleluya! Jambo ndilo hilo. Usiwe na shaka. Simama moja kwa moja. Amina. Bwana asifiwe. Unaweza kuwachukua *hawa*, nao watapata afya, pia. Msitie shaka. Toka moja kwa moja na uwe huru. Bwana asifiwe. Hilo ni jema. Amina.

²⁵⁹ Hebu tuinue mikono yetu sasa, na tumpe Mungu sifa, kila mtu. Umeponywa...?... Mbona, hivi hujaponywa? Katika Jina la Bwana Yesu...?... 

60-0712 Msikieni Yeye
Shule Ya Sekondari Ya Juu Ya Klamath Union
Klamath Falls, Oregon Marekani

SWAHILI

©2026 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org